**Serikali** yasikia kilio, Sheria ya Ndoa kufumuliwa

UKURASA 2



**Waziri** aagiza tathmini gharama kuunganisha maji

UKURASA 3


# Nipashe

Jumatano Julai 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JA I

ISSN 0856 • Na. 0580634

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**PSG, Man City zamgombea Messi**

UKURASA 20



BAA LA CORONA

# Bugando yahitaji mitungi gesi 500

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### WATU 11,000 KUPATA AJIRA UJENZI WA SGR

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amesema mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha...

UKURASA WA 3

### BIL. 1.6/- ZA NHIF ZATAFUNWA VITUONI

ZAIDI ya Sh. bilioni 1.6 za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), zinadaiwa kutafunwa kijanja na watu 17 na vituo...

UKURASA WA 5

### MAMIA WAPOTEZA AJIRA MGOGORO WA SHAMBA

KUMEIBUKA mvutano wa kugombea ekari 2,054 za ardhi ya kilimo katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, huku watu...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipewa maelezo na Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Zempeho Manongi (kulia), kuhusu mashine ya kuchakata zabibu, wakati wa mkutano na wadau wa zao la zabibu, jijini Dodoma, jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: OWM**

## Jaji Mkuu atoa hukumu kesi ya bodaboda

UKURASA 5

## Adaiwa kuua mama yake kisa manabii kutomponya

UKURASA 3

**MICHEZO** **NABI AIWAISHA YANGA KAMBINI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Bugando yalia uhaba wa mitungi ya gesi

**Na Richard Makore,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Bugando iliyoko jijini Mwanza, inakabiliwa na uhaba wa mitungi 500 ya kuhifadhi hewa ya Oksijeni kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wenye matatizo ya upumuaji wakiwamo wa corona.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa kikao cha wadau wa kupambana na ugonjwa huo kilichofanyika chini ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Fabian Massaga, alisema kwa sasa wana mashine za kuzalisha mitungi 100 kwa siku huku mahitaji yakiwa mitungi ya gesi 300.

Kutokana na uhaba huo, Dk. Massaga aliwaomba wadau kutoa msaada ili angalau ipatikane mitungi 500 kwa siku itakayotosheleza mahitaji ya wagonjwa katika hospitali hiyo.

"Idadi ya wagonjwa wanaofika hospitalini wanaohitaji mitungi ya Oksijeni ni wengi na hospitali yetu haina mitungi ya kuzalisha kiasi cha kutosheleza, hivyo tunaomba wadau wajitokeze kusaidia ili tuweze kuwahudumia wagonjwa kwa kuwa wagonjwa ni wengi," alisema Dk. Massaga.

Wakati Bugando ikikabiliwa na uhaba huo, Mkoa wa Mwanza umeainisha vipengele saba vitakavyosaidia kujikinga na ugonjwa huo kwa sasa.

Mkuu wa Mwanza, Gabriel alisema mitungi ya gesi kwa ajili ya wagonjwa wa kupumua kwa sasa inauzwa bei ya juu, huku akiwataka wazalishaji kuongeza uzalishaji ili bei ishuke.

Gabriel aliwataka wadau mbalimbali kujitolea kusaidia vifaa zikiwamo ndoo za kunawia mikono, vitakasa mikono na barakoa ili viwekwe kwenye maeneo yenye mikusanyiko zikiwamo stendi za mabasi, shuleni, sokoni na kwenye ofisi za umma.

Miongoni mwa vipengele ambavyo vitasimamiwa na mkoa huo katika kujikinga ni pamoja na kila mmoja kuhakikisha anavaa barakoa, kunawa mikono na kupaka vitakasa mikono.

Awali, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutanchinzibwa, alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni pamoja na homa, kikohozi kikavu na chenye makohozi, mwili kuishiwa nguvu bila sababu, kukosa hisia za harufu, kupoteza hamu na ladha ya chakula.

Dalili zingine ni kuwasha, viungo kuuma, mwili kuuma, kuharisha, tumbo kuuma pamoja na kifua kuuma.

Alisema gharama ya mtungi mmoja wa Oksjeni ni Sh. 45,000 hadi 50,000 na kwamba bado kuna mwitikio mdogo kwa jamii katika kuchukua tahadhari.



Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Kusimamia Uchaguzi wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGO), Flaviana Charles, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu mchakato wa uchaguzi uliofanyika kwa wilaya na mikoa, kuelekea ngazi ya taifa, ambapo viongozi mbalimbali wamekwishapatikana. Kushoto ni Katibu wa Kamati hiyo, Francis Kiwanga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Ajira 11,000 zaja SGR

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, amesema mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Mwanza hadi Isaka, unatarajia kutoa ajira kwa wananchi 11,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini, Gabriel alisema Shirika la Reli (TRC) linaendelea na kampeni maalum ya utoaji wa elimu juu ya ujenzi huo kwa jamii zinazoishi maeneo yanayopitiwa na mradi. Alisema elimu hiyo itawasaidia wananchi kupata uelewa juu ya ujenzi huo na fidia za mradi wakati wa ujenzi.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema wananchi wa maeneo hayo watapata ajira na kuwataka kuwa walinzi wa mradi huo katika kipindi chote cha ujenzi.

"Wananchi wote ambao mradi huu utapita katika maeneo yao, baadhi yao watapata ajira na watalipwa fidia kulingana na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 na niwahakikishie wananchi hakuna ambaye hatapata haki yake," alisema Gabriel.

Aliongeza kuwa serikali itahakikisha hali ya ulinzi na usalama inaimarika katika maeneo yote, lengo likiwa ni kuwanufaisha Watanzania.

Meneja Mradi wa SGR, Machibya Masanja, alisema mradi wa ujenzi wa reli hiyo ya kwanza ni Dar es Salaam-Mwanza (zaidi ya kilomita 1,200) umegawanyika katika vipande vitano.

Alisema kipande cha kwanza cha Dar es Salaam-Morogoro (kilomita 300), kipande cha pili ni Morogoro- Matukupola (kilomita 422), kipande Singida-Tabora (kilomita 371) na kingine cha Tabora-Isaka (kilomita 162).

Alisema mradi wa ujenzi kipande cha tano cha Mwanza-Isaka una thamani ya zaidi ya Sh. trilioni tatu.

# Sheria ya Ndoa kufumuliwa kisa umri wa kuolewa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaifumua Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwenye vifungu vya umri wa mtoto ili kuondoa ukidhani uliopo unaotoa mwanya kwa mtoto wa kike kuolewa chini ya miaka 18.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geoffrey Pinda, aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati wa ufunguzi wa kikao cha kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya mapitio ya Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 uliokutanisha wabunge, wenyeviti wa halmashauri na wanahabari.

Mabadiliko ya sheria hiyo ni kilio cha muda mrefu cha wadau mbalimbali wa haki za watoto na Oktoba mwaka 2019, Mahakama ya Rufani ilitupilia mbali ombi la serikali kuwa sheria hiyo iendelee ilivyo.

Serikali ilikata rufani dhidi ya hukumu ya Mahakama Kuu kwenye kesi ya kupinga baadhi ya vifungu vya sheria hiyo kwa madai kuwa vinamkandamiza mtoto wa kike, iliyofunguliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Msichana Initiative kwa kushirikiana na asasi nyingine.

Pinda alisema kumekuwa na udhaifu katika sheria hiyo, kwani umri wa serikali ni miaka 18, lakini vifungu vya Sheria ya Ndoa Na.13 na 17 ya mwaka 1971 vinaruhusu mtoto kuolewa chini ya umri wa miaka 18.

Alisema mchakato huo ni kufuatia uamuzi wa Mahakama Kuu katika shauri Na.5 la mwaka 2016 na uamuzi wa Mahakama ya Rufani katika Rufani Na.204 ya mwaka 2017 kuhusu vifungu vya 13 na 17 vya sheria hiyo vinavyoruhusu mtoto kuolewa akiwa na miaka 14 na wa kiume anaweza kuoa akiwa na miaka 15 ni kinyume na katiba ya nchi.

"Tunaingia kwenye mjadala mkubwa na ninyi tunawashirikisha kama wananchi wa Dodoma, kwa ajili ya kupitia na kupata namna ya kuitengeneza hii sheria, kumekuwa na udhaifu katika sheria hii...umri unaotambulika na serikali ni 18, lakini kwenye vifungu hivi vinasema anaweza kuolewa chini ya umri wa miaka 18 ambayo ni miaka 14 na 15 kwa majadiliano ama ridhaa ya wazazi," alisema Pinda.

"Unaweza kuona mtihani tulionao tunatakiwa kutafuta kitu ambacho kitawalinda watoto wa kike, lakini vipi kwa wale ambao hawasomi tunapaswa kuwalinda pia ili wanapotaka kuolewa wawe wamefikisha umri wa miaka 18," alisema.

Aidha, alisema wakati mwingine watoto huozeshwa katika umri mdogo hali inayopelekea kushindwa kuhimili mikimiki ya ndoa na uzazi wakiwa na umri mdogo.

"Ndiyo maana majaji wametuambia tutafute namna nzuri ya kuwaelekeza hawa watoto, tunahitaji mawazo juu ya sheria hii, tuko hapa kupokea maoni yenu mbalimbali kuhusiana na hii sheria ilil isilete madhara kwa watoto na lazima iboreshwe," alisema Waziri Pinda.

Awali, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, alisema wanachohitaji ni kupatikana kwa haki ambayo itawasaidia wananchi katika mifumo ya utoaji haki.

"Tunahitaji kulinda haki za wanawake na watoto wa kike katika mifumo ya utoaji haki hasa kwenye sheria hii ya ndoa, tunachohitaji ni maoni kutoka kwa wadau kuhusiana na sheria hii," alisema Mpanju.

## HABARI KITAIFA

## Bilioni 1.6/- za NHIF zatafunwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. bilioni 1.6 za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), zinadaiwa kutafunwa kijanja na watu 17 na vituo vya afya saba mkoani Mbeya ndani ya miaka miwili.

Hayo yalibainika katika uchunguzi uliofanywa kwa ushirikiano baina ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mkoa wa Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema watu binafsi waliobainika kuhusika na ubadhirifu huo walikuwa wakijifanya wanaumwa magonjwa kama kisukari kisha wanachukua dawa nyingi na zenye thamani kubwa wanakwenda kuziuza kwenye hospitali, maduka au vituo vya afya vya watu binafsi.

"Tumebaini watu binafsi zaidi ya 17 ambao nao wamehusika na ubadhirifu wa fedha hizo, watu hao 17 peke yao wamefanya ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 118, jambo hili sisi kama serikali hatuwezi kulivumilia," alisema Homera.

Alisema wameshawataka watu hao pamoja na wamiliki wa vituo vya afya vilivyobainika kufanya ubadhirifu huo ambao wamekiri na wamepewa muda maalum kurejesha fedha hizo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema mbinu hizo zimekuwa zikitumiwa na wamiliki wa vituo vya kutolea huduma za afya jijini Mbeya kufanya ubadhirifu wa fedha za NHIF.

Alisema baadhi wa vituo wamekuwa wakiwalipa fedha kiasi cha Sh. 20,000 watu wenye kadi za Bima ya Afya, ili wawapatie kadi hizo ambazo wao wanazitumia kujaza fomu za NHIF kwa ajili ya kupeleka madai ili walipwe fedha, wakidai wenye kadi hizo wamepewa huduma za matibabu.

Alisema mbinu nyingine ni wahusika kujaza fomu za madai ya kulipwa na NHIF wakionyesha walitoa dawa za gharama kubwa kuliko zile alizopewa mgonjwa.

# Adaiwa kumnyonga mama kisa manabii kutomponya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWANAFUNZI wa kidato cha nne katika shule moja ya sekondari mkoani Kilimanjaro, anadaiwa kumnyonga mama yake mzazi hadi kufa.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kutekeleza mauaji hayo baada ya kuchukizwa na uamuzi wa mzazi wake huyo kumpeleka kwa nabii wa uongo, kutafuta uponyaji wa matatizo ya kiafya yanayomkabili.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Amon Kakwale, alithibitisha kukamatwa na kushikiliwa kwa mwanafunzi huyo kwa ajili ya mahojiano kuhusiana na mauaji hayo ya mama yake.

"Ni kweli kuna hayo mauaji ya mama kunyongwa na mwanawe wa kumzaa. Taarifa kamili nitaitoa kesho (leo)," alisema Kamanda Kakwale.

Mtuhumiwa huyo ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Kindi iliyoko Moshi Vijijini, anadaiwa kutekeleza mauaji hayo usiku wa Julai 5, mwaka huu.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sambarai kilichoko Kata ya Kindi, Wilaya ya Moshi, Josephine Masenga alisema:

"Nilipigiwa simu jana (juzi) asubuhi na mmoja wa wana kijiji wangu, baada ya kumwona mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) akiwa na damu miguuni huku akiongea lugha zisizoeleweka.

"Nilifika eneo la tukio, tulikuta mazingira yenye utata, tukajaribu kumwita mama huyo, mara kadhaa bila mafanikio, huku damu zikionekana kuchuruzika mlangoni.

"Ndipo nilipopiga simu polisi na wakaja, walivunja nyumba na tukamkuta mama huyo amefariki dunia.

"Siku ya Jumapili tukiwa katika misa ya kwanza, huyo mwanafunzi alifika kanisani (Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi, Kigango cha Sambarai) na kutaka kukimbilia altareni (madhabahuni), lakini alishikwa na kutolewa nje.

"Anasema alichukia kwa sababu mama yake alimpeleka katika maombi ya kinabii huko KCMC (Kata ya Longuo, Manispaa ya Moshi) lakini hakuyaelewa na anaona kama kuna mchezo wa kuigiza."

Hata hivyo, baadhi ya majirani, akiwamo Faustina Mallya, walidai mama huyo waliyemtaja kwa jina la Marieta, wakati wa uhai wake alikuwa ana ulemavu wa mkono na mguu.

"Hatujui ni nini kimetokea, hatukusikia kelele yoyote, ingawa jana binti huyo alipotolewa kanisani, alianza kubishana na mama yake, akionekena kukataa kupelekwa eneo ambalo hatukujua ni wapi," alisema Faustina.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kindi, Clemence Mushi, anakosoma mtuhumiwa wa mauaji hayo, alisema haelewi kilichotokea kwa vile huwa anamwona mwanafunzi huyo mpole, mtii na mwenye nidhamu.



Waziri wa Maji, Juma Aweso (wapili kulia), akimkabidhi Tuzo ya Utendaji Bora katika Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (DAWASA) Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto), wakati wa hafla ya kujadili huduma za maji kwa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam jana. Katikati ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, (kulia) ni Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA, Jenerali mstaafu, Davis Mwamunyange. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri Aweso aagiza tathmini gharama kuunganisha maji

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema haridhishwi na gharama za kuwaunganishia huduma za maji wananchi, hivyo aliziagiza mamlaka za maji nchini, kufanya tathmini ya gharama hizo.

Amesema lengo la hatua hiyo ni kuja na gharama ambazo hazitamuumiza mwananchi.

Agizo hilo alilitoa jana mkoani Dar es Salaam kwenye mkutano ulioandaliwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) wa kufanya tathmini ya huduma ya majisafi na salama Dar es Salaam na Pwani imefikia wapi.

Alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye miradi ya maji katika maeneo mbalimbali, lakini haridhishwi na gharama za uunganishwaji huduma za maji kwa wananchi.

"Siridhishwi na gharama za kuunganisha maji kwa wananchi, nataka mje na standard, mwanachi ili kuunganishiwa maji ni kiasi gani? Na kumuunganishia maji mwananchi inajulikana...itahitajika chemba, mabomba, uzuri sasa hivi viongozi wetu wamewekeza viwanda ni vingi na hata gharama za mabomba sio kubwa," alisema na kuongeza:

"Naomba mje na gharama halisi, na hili jambo naomba DAWASA mkalifanyie kazi, muweze kutusaidia sisi kama wizara ili tuje na gharama moja kuwa mwananchi ili kuunganishiwa huduma ya maji anahitaji kulipia gharama kadhaa."

Katika mkutano huo, ulioshirikisha viongozi kutoka mikoa wa Dar es Salaam na Pwani, wakiwamo wabunge, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya pamoja na wakurugenzi, zilitolewa zawadi kwa wafanyakazi wa DAWASA waliofanya vizuri. Waliokabidhiwa ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa mamlaka hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja na fundi Erasto Majuto aliyepewa zawadi kwa kujitoa kwake kuhudumia wananchi.

Erasto Majuto picha yake ilipostiwa kwenye akaunti za mitandao ya kijamii ya Nipashe ikimwonyesha akiziba bomba lililopasuka ndani ya shimo, huku mvua kubwa ikinyesha.

Wakati wa tukio hilo la zawadi, Rais Samia Suluhu Hassan alipiga simu na kutoa taarifa kuwa nafuatilia tukio hilo kwenye televisheni, na kuvitiwa kwa jinsi wafanyakazi wa DAWASA walivyojitoa kuhudumia wananchi na kuwaahidi yupo pamoja nao hivyo wasimwangushe.

Aweso ndiye aliyetoa salama hizo za Rais Samia kwenye mkutano huo, alisema "Rais Samia anafuatilia mkutano huu anawapenda na amesema yupo pamoja na nyie na msimwangushe, amesema ameona kuna watendaji wazuri wakiwamo kina Majuto, aliyezama kwenye dimbwi la maji ili kuhakikisha wanadhibiti upotevu wa maji."

RIPOTI MAALUM -3

## USUGU SHIDA YA AJIRA

# CAG alia ugumu katika uwekezaji

Na Sanula Athanas

***SEHEMU ya pili jana iliangazia hali ya ajira katika awamu za pili na tatu, huku Rais Samia Suluhu Hassan akianika takwimu za waajiriwa nchini. Endelea na sehemu ya mwisho.***

**MWANAZUONI AIBUA YAKE**

Hoja iliyojengwa na Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Benjamin Mkapa, iliyonyooshea kidole ongezeko la watu lisilowiana na ukuaji uchumi, kwamba ni tatizo, inaungwa mkono na mwanazuoni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Dk. Darius Mukiza, Mhadhiri wa Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma katika chuo hicho, anamuunga mkono Rais Mkapa kwamba idadi ya watu ni mzizi wa tatizo la ajira nchini.

Anafafanua hoja yake kwa kurejea kilichofanyika China miongo minne iliyopita, ilipodhibiti idadi ya watu wake, anayoielezea sasa ni ukombozi dhidi ya shida ajira.

**ZAMA ZA JK**

Awamu ya Nne chini ya Rais Jakaya Kikwete, ilikuwa na miradi mingi ya maendeleo iliyozalisha ajira za moja kwa moja.

Alipoingia madarakani mwaka 2005, Rais Kikwete aliuendeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) uifikie kila kata, hatua iliyofungua mapana ya ajira za kudumu katika Sekta ya Elimu.

MMES ilifungua ajira kwa kuhudumia shule zake kupitia watumishi shuleni, wajenzi na biashara zinazogusa shule.

Mwaka 2008, ulianza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) na kushuhudiwa zahanati, vituo vya afya na hospitali nyingi kutanuliwa.

Pia, ndicho kipindi miradi mingi ya ujenzi wa barabara ilishuhudiwa kitaifa. Yote hayo yalifungua fursa za ajira.

Aina ya yaliyojiri katika awamu ya nne, ndicho kiliendelezwa chini ya Rais John Magufuli, kikiendana na miradi mipya. Zao lake ni ajira zinazotangazwa sasa.

Hata hivyo, awamu ya tano ilisitisha ajira serikalini kwa takriban miaka mitatu kupisha ukaguzi wa vyeti na watumishi hewa.

**ANACHOBAINI CAG**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) haiko nyuma katika tathmini ya uhaba wa ajira kitaifa.

CAG, Charles Kichere, kupitia ripoti ya 2019/20 iliyowalishwa bungeni Aprili mwaka huu, anasema kupungua uwekezaji mpya kumekwaza ajira.

Anabainisha miradi mipya kwenye Kituo cha Uwekezaji (TIC) ilipungua kwa wastani wa nusu na ndiyo ulikuwa uhalisia wa mwenendo wa ajira nchini miaka mitano iliyopita.




CAG Charles Kichere. **PICHA: MTANDAO**

**JEDWALI LA HALI YA USAJILI WA MIRADI NCHINI**

| Mwaka | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| Miradi iliyosajiliwa | 420 | 352 | 274 | 272 | 219 |
| Thamani (Dola mil.) | 7,716.39 | 2,777 | 2,285 | 2,577.57 | 1,853.47 |
| Ajira zilizozalishwa | 63,223 | 26,051 | 33,702 | 48,102 | 32,115 |

Kupungua kwa miradi mipya iliyosajiliwa TIC kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20. **CHANZO: Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2019/20**.

CAG anasema ndani ya kipindi hicho, ajira zilipungua kutoka waajiriwa 63,223 mwaka 2015/16 hadi waajiriwa 32,115 mwaka 2019/20, sawa na asilimia 48.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, anazitafsiri takwimu hizo kwamba zinakinzana na maelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17- 2020/21.

Utouh ambaye ni CAG mstaafu, anauainisha mpango huo unaielekeza serikali kuhamasisha, kuwezesha na kuratibu uwekezaji, mabadiliko ya teknolojia, viwanda na biashara nchini.

Ripoti ya CAG inasema kupungua miradi hiyo kumechangiwa na kuwapo mazingira hasi kwa uwekezaji.

Inabainisha Tanzania kuwa ya 141 kati ya nchi 190 kwa vigezo vya mazingira rafiki kwa uwekezaji na inatajwa kuporomoka kwa asilimia nane, katika utengenezaji mazingira rafiki ya uwekezaji kwa miaka mitano iliyopita (2015-2020).

CAG anasema ni hali inayosababishwa na TIC kutotoa huduma zote stahiki za uwekezaji (one stop centre), ikitoa huduma nne kati ya 11 zinazotakiwa kuwapo.

"Kuna ucheleweshaji wa mrejesho wa maombi ya uwekezaji katika mamlaka husika. Vigezo vya kimataifa vinataka iwe ndani ya siku 14, lakini uhalisia uliopo nchini ni siku 182 hadi 675," anabainisha.

Ni hali inayotoa tafsiri kitaalamu kwamba hitaji la wiki mbili, linahitimishwa ndani ya wiki 26 au miezi sita.

CAG anadokeza Tathmini ya Athari za Mazingira inayotekelezwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), inachukua muda mrefu kukamilika, wastani wa siku 95.

Vilevile, ananyoshea kidole uhaba wa bajeti, akibainisha upungufu wa nusu ya hitaji halisi ambayo ni Sh. bilioni 45 (asilimia 49 ya mahitaji) na uhaba wa theluthi moja ya watumishi (asilimia 35 ya mahitaji ya watumishi 513) kwa mwaka huo wa ukaguzi.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Mei 4 mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, aliliarifu Bunge jijini Dodoma kwamba serikali inatarajia kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa lengo la kuhakikisha inakidhi mahitaji ya sasa.

Alisema serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini ya kina ya mitaala inayotumika kwa sasa ili kuhakikisha ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa kuzingatia viwango na vigezo vilivyowekwa.

Alisema lengo ni kuweka msisitizo zaidi katika ufundishaji wa masomo ya ufundi kwa kuimarisha mafunzo kwa vitendo ili kuwa na wahitimu wanaomudu ushindani wa soko la ajira na watakaojiajiri wanapokosa nafasi za kuajiriwa.

"Serikali itaanza kufanya mapitio ya mitaala katika ngazi zote za elimu ili kuhakikisha elimu na mafunzo yanayotolewa yanajikita katika kujenga ujuzi na kuzingatia mahitaji ya sasa," alisema.

Ofisi ya Waziri Mkuu ilibainisha bungeni wiki iliyopita kuwa serikali imeandaa mikakati minane ya kukabiliana na uhaba wa ajira nchini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ummy Nderiananga, alianika mikakati hiyo alipojibu swali la Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Mathayo, aliyehoji kama serikali ina mkakati mahusussi wa kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wanapohitimu vyuo vikuu.

"Je, ni kwa nini vijana hao wasitumie vyeti vyao kama dhamana kupata mikopo ili wajishughulishe na shughuli mbalimbali za kiuchumi?" Mbunge huyo alihoji.

Naibu Waziri Nderiananga alisema serikali imeandaa mkakati wa kitaifa wa kukuza fursa za ajira ambao unatoa maelekezo kwa sekta zote za kiuchumi ya namna sekta hizo zinavyopaswa kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji ili wawekeze na kuzalisha fursa za ajira za kutosha.

Alitaja mikakati mingine ni serikali kuanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu.

"Katika kipindi cha miaka mitatu, jumla ya wahitimu 5,975 wamewezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi kwenye taasisi mbalimbali za umma na binafsi ikiwa ni mkakati wa kuondoa kikwazo cha uzoefu kwa vijana wanapotafuta kazi," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya ufundi na stadi katika fani mbalimbali kwa vijana wakiwamo wahitimu wa elimu ya juu ambapo katika kipindi cha miaka mitatu, jumla ya vijana 28,941 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kupitia mafunzo ya uanagenzi.

"Serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo usio rasmi wa mafunzo kwa lengo la kuwawezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri na pia kujiendeleza kiujuzi katika taasisi mbalimbali za mafunzo," alisema.

Vilevile, alisema serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa vijana wakiwamo wahitimu wa elimu ya juu kupitia teknolojia ya kitalu nyumba.

"Serikali imetekeleza programu ya vijana kufanya mafunzo ya uzoefu wa kazi katika sekta ya kilimo kwa kuwapeleka katika nchi ambazo zimepiga hatua katika kilimo ambapo katika mwaka uliopita tumegharamia vijana 136 kuhudhuria mafunzo Israel.

"Vilevile, serikali imeanza kufanya utafiti kuhusu hali ya ajira nchini," alisema na kubainisha kuwa serikali inapokea ushauri mbunge huyo wa kutumia vyeti vya kuhitimu mafunzo kama dhamana ya mikopo kwa vijana na inakwenda kuufanyia kazi.

Nderiananga alisema serikali imeendelea kuboresha huduma ya utoaji mikopo kwa vijana kupitia mifuko na programu mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi," alisema.

Kwa Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inashughulikia masuala ya sera, ajira, kazi, vijana na uwekezaji.

## Adaiwa kuua mke na mtoto akidai fedha za matunzo

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita linamshikilia, Petro John, mkazi wa kijiji cha Masota, wilayani Bukombe kwa tuhuma za mauaji ya Esther John (28) na mtoto wake, Winfrida Masumbuko (13) kwa madai ya kushindwa kumlipa gharama za matunzo alizotumia wakati huo akiwa mpenzi wake.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya mauaji hayo kisha kuwazika porini eneo la mashamba ya mpunga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alisema tukio hilo lilitokea Juni 18, mwaka huu na katika mahojiano na Jeshi la Polisi mtuhumiwa huyo, alisema aliamua kudai hela ya matunzo kutoka kwa mpenzi wake kwa kuwa alihisi mkewe alikuwa amepata mpenzi mwingine.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Juni 29, mwaka huu, na baada ya kukiri kutenda tukio hilo alikwenda kuwaonyesha polisi alipoizika miili hiyo.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, mtuhumiwa amedai kwamba Ester alikuwa mpenzi wake na katika kipindi kirefu alikuwa akimhudumia kwa gharama kubwa, na kwamba alimuomba amrudishie gharama hizo.

Aliongeza kuwa Ester alishindwa kurudisha gharama hizo, ndipo mtuhumiwa siku ya tukio alimwomba akamsaidie kuvuna mpunga, lakini wakiwa njiani alimshambulia na kumuua.

Aidha, ilidaiwa mtuhumiwa aliamua kuumua mtoto wa Ester ili kuficha ushahidi wa mauaji ambayo yalitekelezwa siku hiyo hiyo katika eneo la mashamba ya mpunga.

# Jopo la Jaji Mkuu latupa rufani ya bodaboda aliyepora abiria

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani ya Tanzania imetupilia mbali rufani iliyokatwa na bodaboda, Athumani Musa, akipinga kufungwa miaka 30 kwa kumpora abiria wake vitu mbalimbali kwa kutumia silaha.

Mahakama imesema haiwezi kutoa uamuzi tofauti na uamuzi wa mahakama mbili za chini, na kwamba adhabu hiyo ni ya chini haiwezi hata kupunguzwa.

Uamuzi wa Mahakama hiyo ulitolewa juzi na jopo la Majaji watatu, Prof. Ibrahimu Juma, Rehema Mkuye na Jaji Barker Sahel.

Katika uamuzi jopo hilo linasema kwamba ushahidi wa pande zote mbili umezingatiwa, na kwamba mahakama za chini hazikuzungumzia utetezi, kwa sababu ushahidi wa utetezi haukuwa na nguvu.

"Ushahidi wa upande wa Jamhuri hauna shaka yoyote, mrufani aliegemea kuzungumzia jinsi alivyokamatwa badala ya kuangalia ushahidi wa Jamhuri dhidi yake.

"Mahakama mbili za chini, Mahakama ya Wilaya ya Kigoma na Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma zilikuwa sahihi katika kutoa uamuzi, Mahakama hii haiwezi kutoa uamuzi tofauti, adhabu ya miaka 30 jela ni adhabu ya chini, haiwezi kupunguzwa," lilisema jopo hilo na kuitupilia mbali rufani iliyokatwa dhidi ya Jamhuri.

Katika kesi hiyo mrufani alijiwakilisha mwenyewe, huku Jamhuri ikiwakikishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Adolf Maganda, Yamiko Mlekeno na Wakili wa Serikali Shabani Masanja na Happiness Mayunga.

Athumani alitiwa hatiani na Mahakama ya Wilaya Kigoma kwenda jela miaka 30 kwa unyang'anyi wa kutumia silaha, tukio ambalo alilifanya Agosti mwaka 2018.

Inadaiwa alipokodiwa na Jamila Sadiki ampeleke sokoni majira ya jioni, mrufani alimpeleka, Jamila alimpa fedha bodaboda huyo akaenda kumnunulia chumvi na kurudi baada ya dakika kadhaa.

Jamila katika ushahidi wake anadai walipotoka kununua chumvi alimwambia anrudishe nyumbani Kiganza, lakini badala ya kwenda huko alimpeleka njia tofauti maeneo ya Kigoma Mjini.

Anadai alifika mahali akasimamisha pikipiki, wakatokea watu wanne na kimvamia Jamila, wakiwa na kisu, huku mwingine akimtaka asali sala yake ya mwisho.

Jamila alisali sala ya mwisho, akaporwa simu aina ya Nokia yenye thamani ya Sh. 350,000 na fedha taslimu Sh. 40,000, wakati wakifanya hivyo, walimjeruhi kwa kisu.

"Nilimsikia mrufani akisema kwamba kamanda nimeshampeleka, nimemaliza, malizeni tufute ushahidi," alidai Jamila katika ushahidi wake.

Mahakama ya Wilaya baada ya kusikiliza ushahidi huo na mwingine, ilisikiliza pia utetezi ambapo mshtakiwa alikuwa akikana kutenda kosa hilo, ilimtia hatiani mshtakiwa na kumuhukumu kwenda jela miaka 30.

Mshtakiwa hakukubaliana na adhabu hiyo alikata rufani Mahakama Kuu mbele ya Jaji Athumani Matuma akashindwa, ndipo alipokimbilia Mahakama ya Rufani.



Ofisa Mwandamizi wa Forodha, Chrisant Kyomushula (wapili kulia), akifafanua jambo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Suleiman Missango (wapili kushoto), jinsi K ituo cha Pamoja cha Huduma Mpakani kinavyofanya kazi, alipotembelea Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere juzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mamia wapoteza ajira mgogoro wa shamba

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUMEIBUKA mvutano wa kugombea ekari 2,054 za ardhi ya kilimo katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, huku watu 600 wakipoteza ajira.

Mgogoro huo unahusisha wawekezaji watatu wa kigeni na kampuni moja ya kizalendo ya Tudeley Estates Limited.

Kutokana na mgogoro huo, wafanyakazi 600 tayari wamepoteza ajira zao, huku vyama vinne vya ushirika wa mazao (AMCOS) vinavyounda Muungano wa Vyama vya Ushirika vya MUROSOSANGO vikimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati kutafuta ufumbuzi wake.

Jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya Tudeley Estates Limited iliyoingia ubia na Kampuni mama ya Tudeley Holdings Limited ya Uingereza kuendesha mashamba mawili yaliyopo eneo la Kibohehe, Jenseen Natai, alisema mgogoro huo umesababisha wawekezaji hao kutelekeza mali zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni saba.

"Kuna wawekezaji wanne wanadai wamewekeza ndani ya hili shamba sasa hivi, kuna Muingereza (Tudeley Holdings Limited) wameotesha kahawa karibia ekari 400, wamechimba mabwawa na mabomba yapo.

"Balton ambao ni Waisrael, wameweka mfumo wa umwagiliaji shambani ambao nao una thamani ya zaidi ya bilioni moja. Wajerumani nao wanadai wameotesha parachichi ekari 200, na pesa nyingi waliweka huko.

Bahati mbaya, Watanzania nao wamelima mahindi, maharage ambayo yana thamani ya karibia Sh. bilioni moja tena. Hili shamba kwa kipindi kama hiki tulizoea kuajiri watu 500 hadi 600 wakati wa kuchuma kahawa, lakini sasa hivi tuna wafanyakazi hawazidi 60.

"Kuna nafasi ya serikali hasa kwa Rais wetu kuwakutanisha pamoja au kuangalia taratibu na kushauri pande zote, kwa sababu suala la mataifa ya nje nadhani litahitaji ungalifu," alisema.

Katibu wa Muungano wa Vyama vinne vya Ushirika vya MUROSOSANGO, Jubilate Ndossi, alisema wakulima kutoka Vyama vya Masama Roo AMCOS, Sau AMCOS, Mudio AMCOS na SonuNgira, wanachopambania kwa sasa ni serikali kumaliza mgogoro huo ili mashamba hayo yaendelee na uzalishaji wa kahawa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwandani na Kilimo (TPAWU), Tawi la Tudeley, Yohana Ernest, alisema wafanyakazi wa mashamba hayo wanafanya kazi kwa zaidi ya miezi sita hadi saba bila kulipwa ujira wowote.

Machi 5, 2019, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (sasa Makamu wa Rais) na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, walieleza nia ya serikali kumuita mwekezaji wa Kampuni ya Tudeley Estates Ltd, Conrad Leg ambaye aliingia mkataba na vyama vinne vya ushirika vinavyounda Ushirika wa MUROSOSANGO.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Polisi iongeze nguvu kudhibiti uhalifu huu

**JESHI** la Polisi limetangaza kufanikiwa kunyamazisha ujambazi uliokuwa umeanza kuibuka kimya kimya kwenye maeneo mengi nchini, hii ni habari njema.

Na kwamba miji ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza iliyotishiwa na wimbi la ujambazi hivi karibuni iko salama baada ya operesheni ya kwanza kupambana na majambazi kufanikiwa kwa ufanisi. Aidha, pamoja na taarifa hizo, polisi inawaonya wanaodhani kuwa kufanya ujambazi ni njia sahihi ya kujipatia kipato waache tabia hiyo.

Lakini, si majambazi pekee inatoa karipio kali kwa hata wale wanaotumia pikipiki kupora ikitaja matendo hayo kuwa ni makosa makubwa na anayekamatwa askari watamalizana naye kimya kimya na kutaka Watanzania kufanyakazi halali kupata kipato halali.

Hata hivyo, kauli ya serikali inakuja wakati kwenye maeneo mengi ujambazi na wizi mdogo mdogo ni kero kubwa. Uhalifu huo ukihusisha uporaji wa kutumia pikipiki ambao umerejea kwa kasi na inavyoelekea unahitaji nguvu na operesheni zaidi kupambana.

Wizi huo unawaibia watu pochi, mikoba na simu kwenye vituo vya daladala, barabarani, mitaani hasa kwenye uficho lakini hata ndani ya vyombo vya usafiri.

Malalamiko ni mengi yakiwamo ya wizi wa vioo vya magari na vifaa vingine hasa barabarani wakati wa foleni. Jambo hili linaashiria kuwa siyo wakati wa kujisifu kumaliza tatizo la ujambazi wakati wizi na udokozi unazidi kukithiri.

Mathalani, maeneo mengi ya Dar es Salaam watu wanalalamikia kuibiwa runinga 'flat screen' nondo za madirisha huvunjwa na TV pamoja na vitu vingine huibwa.

Hivi karibuni limetokea tukio eneo la Temeke waliingia nyumbani kwa mtu na kujaribu kuiba gari, lakini wahusika waliwashtukia mapema, huku matukio ya watu kuibiwa vifaa vya magari yakiongezeka kwa kasi.

Si hivyo tu kuna madai kuwa wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro, maeneo ya Kaseni, Kifula, Kisanjuni na Msangeni umeingia wizi mpya wa kuvunja madirisha kupuliza dawa za usingizi na kuiba vitu vya ndani kama TV, simu na mali nyingine za thamani.

Katika eneo hilo kumekuwa na matukio sita yaliyoripotiwa kutokea kwenye nyumba mbalimbali za wakazi wa eneo hilo.

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, lilieleza kuhusu kukamata zaidi ya watuhumiwa 100 wa wizi wa vifaa vya magari na vyombo vya usafiri na kuonyesha vifaa vingi walivyodai vimeibwa maeneo mbalimbali.


Pamoja na hayo bado wizi unaripotiwa Tegeta, Salasala, Boko, Mikocheni na Tabata na kwa sasa ni kawaida mnapokuwa watu 10 kwenye kundi, watatu au wanne utawasikia wakieleza kuwa na matukio ya wizi kwenye nyumba zao yanatisha.

Tunaona kuwa siyo jambo jema kwa jeshi hilo kujisifu, ndiyo maana tunashauri mbinu zilizotumika kudhibiti hali hiyo kwa miaka iliyopita zitumike tena kuhakikisha matukio haya yanakuwa historia. Tunaona kuwa ni wakati wa kuimarisha kikamilifu polisi jamii na kudhibiti uhalifu kwenye mitaa mbalimbali, ikiwamo kuwapa walinzi motisha, vitendea kazi pamoja na kuwatumia askari wa pikipiki, kufanya doria na hata ikibidi kura za kuwatambua wahalifu.

Pamoja na hayo ni vyema Watanzania wakakumbuka kuwa wajibu wa ulinzi wa nchi ni jukumu lao kikatiba na kushirikiana na polisi ambayo ni taasisi ya dola yenye wajibu wa kulinda raia na mali zao na kuwapa ushirikiano wa kufichua uhalifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

## Saratani ya matiti isiachiwe kuendelea kuua wanawake

Na shamila Ramadhani, SJMC

**MIAKA** ya hivi karibuni imeshuhudia ugonjwa wa saratani ya matiti ukiibuka kwa kasi kiasi cha kuwa tatizo kubwa linalotishia maisha katika mataifa ya Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara tofauti na hali ilivyokuwa hapo awali.

Kutambulika kwa tatizo hili kwa wanawake wengi kumechangiwa na kukua kwa sayansi na teknolojia na hasa kuwapo na vifaa au mashine za kisasa za kufanya utambuzi wa tatizo hilo kuanzia 'ultra sound', CT na pet skani'.

Ni ukweli unaotia uchungu kuwa kinamama wengi wamepoteza maisha kwa miaka mingi ya nyuma na hata sasa kutokana na ugonjwa huo, lakini ukosefu wa elimu ya wazi kuhusu utambuzi wa tatizo hilo mapema na kuwahi hospitalini.

Zama hizi zilizoimarika kitabibu kutokana na kukua kwa teknolojia na hasa katika eneo la matibabu na taarifa zake kupatikana kwa wingi kwenye mitandao ya kijamii, redio na runinga, wanawake wengi wana nafasi ya kupata maelezo sahihi na ya haraka kuhusu namna bora ya kujichunguza, kujilinda, kujitambua na zaidi kupata tiba ya kansa ya matiti mapema.

Hata hivyo, wakati baadhi ya maeneo yakifurahia kukua kwa sayansi na teknolojia, na hasa kwa upatikanaji wa maarifa na taarifa za tatizo hilo kwa haraka, bado kampeni juu ya maradhi hayo zimekuwa ndogo kwa maeneo ya vijijini.

Ni kwa sababu kumekuwapo na matukio ya wanawake wengi kujitokeza hadharani wakiomba msaada kwa serikali na wadau mbalimbali hata watu binafsi ili waweze kupatiwa matibabu ya saratani hiyo.

Hata hivyo, wengi wa waathirika wa shida hiyo wanaonekana tayari wameshaelemewa na tatizo hilo ambalo limewaumiza kwa kiasi kikubwa na kuathiri mwili kwa muda mrefu.

Matukio kama hayo yanaonyesha kuwa wengi wao huenda hawajapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu kujilinda na kujichunguza afya.

Wapo watu wazima, kinamama wenye umri wa makamo lakini hata mabinti. Tatizo linaloashiria kuwa kundi kubwa kwenye jamii bado halifahamu kikamilifu kuhusu ugonjwa huo.

Ni wakati kwa serikali kupitia Wizara ya Afya na kushirikiana na wadau kuongeza wigo wa kampeni za kuelimisha umma kuhusu tatizo hili ili wanawake wengi waweze kunufaika na upatikanaji wa taarifa sahihi na za haraka na kupatiwa matibabu.

Ni wazi kuwa iwapo wanawake wengi wataelimika na kufahamu kuhusu ugonjwa huo watakuwa kwenye nafasi ya kujilinda na kuepusha uwezekano mkubwa wa saratani hii kuumiza watu wengi zaidi.

Kuwapo kwa ufahamu kutapunguza kulifanya tatizo hili la kansa kuwa kubwa zaidi na kuwaumiza wanawake ambao wanakuwa kwenye nafasi ya kutotibika.

Dalili za kansa ya maziwa ni uvimbe kwenye titi, au kwapani, kuvimba titi zima, chuchu kuwa na rangi nyekundu na wakati mwingine kunywea na kuzama ndani.

Pamoja na saratani ya matiti shida nyingine kwa kinamama ni kansa ya shingo ya kizazi ambayo kwa upande mwingine ni kitisho kwa afya ya wanawake na mabinti nchini.

Baadhi ya dalili za maradhi hayo ni kupata hedhi baada ya kukoma siku za mwezi, kuwa na hedhi za vipindi virefu na kutokwa na damu nzito na nyingi, kupata maumivu baada ya tendo la ndoa na kuongezeka uchafu unaotoka sehemu za siri.

Kinamama wasichoke kufuatilia na kufahamu hali ya afya zao ili kujikinga na maradhi hayo.

HABARI KITAIFA

# TAMISEMI yataja mafanikio lukuki siku 100 za Samia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeeleza mafanikio yake katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alitaja mafanikio hayo ni katika maeneo ya huduma za afya, sekta ya elimu msingi na sekondari, miundombinu ya barabara, utawala na usimamizi wa mapato ya ndani ya halmashauri.

Alisema serikali imepeleka Sh. bilioni 20.3 kwenye halmashauri 34, kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri. Pia halmashauri 76, zimepelekewa Sh. bilioni 11 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu 3 kwenye kila halmashauri.

Vile vile, kupitia mradi wa matokeo ya ufanisi umefanyika uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya, kwamba zahanati 279, vituo vya afya 46 na hospitali 22 za wilaya zimepatiwa Sh. bilioni 30.

Ummy alisema kupitia mfuko wa pamoja wa afya Sh. bilioni 1.6 zimetolewa kwa ajili ya kununua vifaa tiba vya usingizi katika vituo vya afya 32, ili kuviwezesha vituo hivyo kufanya upasuaji ikiwamo upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni.

Aidha, alisema kupitia Mradi wa 'Commodity Import Support', serikali imewezesha ujenzi wa vituo vya afya 20, katika halmashauri 20 na kila kituo kimepatiwa Sh. milioni 500.

Alisema katika kipindi hicho, serikali imefanikiwa kuajiri watumishi 2,726 wa afya wakiwamo madaktari, wauguzi na wataalamu wa maabara.

Pia alisema serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia, kwamba Sh. bilioni 152.1 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa vya shule za msingi na sekondari.

Kadhalika, alisema Sh. bilioni 17.5 zimetolewa na kupokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya maabara 582 za sayansi katika halmashauri mbalimbali nchini.

"Pia kiasi cha Sh. bilioni 8.8 kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 110 kwa baadhi ya shule za sekondari zenye changamoto ya wanafunzi kutembea umbali mrefu," alisema Ummy.

Vile vile, alisema serikali imetoa kiasi cha Sh. bilioni 83.2 kwa ajili ya kugharamia elimu bure. Hata hivyo alisema katika kuboresha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi, imeajiri walimu 6,946 wa shule za msingi na sekondari.

"Katika kipindi hiki cha siku 100 walimu 119,887 waliotimiza vigezo walipandishwa madaraja kati ya 122,574 waliokasimiwa sawa na asilimia 97.8 na walimu 622 walisajiliwa na kupatiwa namba ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)," alisema Ummy.

Alisema Sh. bilioni 37.6 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya kilometa 3,357.14.

# PM akoleza moto uzalishaji zabibu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka halmashauri za Mkoa wa Dodoma kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche ya zabibu, ili kuwezesha wakulima kupata mbegu bora na za uhakika.

Aidha, amevitaka vyama vya ushirika wa kilimo cha zabibu kuanzisha vitalu vya miche na kuwawezesha wanachama wake kupata mbegu bora katika maeneo yao kwa urahisi.

Alitoa maagizo hayo jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na wadau wa uendelezaji zabibu.

Pamoja na mambo mengine, Waziri Mkuu alizitaka taasisi nyingine ikiwamo Jeshi la Kujenda Taifa (JKT) na Jeshi la Magereza kuanza kulima zao hilo kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima wengine.

"Pia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia kituo chake cha Makutupora iimarishe utafiti wa zao hili ili kupata miche bora na yenye tija na kuifikisha kwa wakulima," alisema Majaliwa.

Vile vile, alisema kupitia kampeni ya kuendeleza zao hilo, serikali itasimamia, kuhakikisha zabibu inayolimwa nchini inakuwa na ubora lengo likiwa ni kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema kwa sasa Wizara ya Kilimo imeanza usajili wa wakulima wa zabibu ili waweze kuwatambua na kuwafikia kwa urahisi.





**Tangu kampuni ya Barrick** ilipoingia ubia na Serikali ya Tanzania, mwaka 2019, ilijikita katika kufufua na kukuza uzalishaji katika migodi ya North Mara, Bulyanhulu na Buzwagi. Kwa hakika, jitihada hizo zilizaa matunda. Kwani, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2020, kampuni ya Barrick iliweza kuilipa Serikali gawio la Dola Milioni 250 pamoja na awamu ya kwanza ya Dola Milioni 300 kama malipo yaliyotokana na maafikiano (settlement) na Serikali. Aidha, kampuni ya Barrick imewekeza Dola Milioni 800 katika uchumi wa nchi na kutumia kiasi cha Dola Milioni 2 katika masuala mbalimbali ya kijamii. Kwa upande wa raslimali watu, Barrick, imetengeneza ajira mpya 600. Hatua hii imefanya asilimia 96 ya wafanyakazi wote migodini kuwa ni Watanzania.

Upande wa uzalishaji, kuna uwekezaji mkubwa unaofanywa katika migodi ya North Mara na Bulyanhulu ili kuiwezesha migodi hiyo, kufikia hatua ya daraja la hali ya juu kabisa ya uzalishaji wa dhahabu (**Tier 1 Gold Complex*). Hatua hii, itaifanya migodi ya Barrick yenye hadhi hiyo duniani kuwa saba.

dPA 647

BARRICK
Tunajenga Mustakabali
www.barrick.com | NYSE : GOLD · TSX : ABX

* *Mgodi wa daraja la juu (Tier One Gold Asset), ni mgodi wenye uwezo wa kuzalisha wakia 500,000 za dhahabu kwa mwaka kwa gharama iliyo chini ya wastani wa gharama za uzalishaji katika sekta ya madini ya dhahabu kwa kipindi cha wa uhai wa mgodi huo ambao ni angalau miaka kumi.*

26348202

HABARI KITAIFA

# TARI yaainisha mikoa mitatu uzalishaji alizeti

**Na Ashton Balaigwa**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imeainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa kilimo cha alizeti nchini, baada ya udongo wake na hali ya hewa kufaa katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu, ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula.

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI, Mlingano, Dk. Catherine Senkolo, aliyasema hayo jana wakati akitoa maelezo kwa wananchi waliotembelea banda la TARI katika viwanja vya Maonyesho ya SabaSaba, Dar es Salaam.

Mkurugenzi huyo alisema wameamua kuainisha maeneo hayo kwa ajili ya kusaidia taasisi au wafanyabiashara wakubwa wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye kilimo cha zao hilo.

Alisema kwa sasa nchi inakabiliwa na upungufu wa mafuta ya kula na kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi, na kwamba kama uwekezaji huo utafanyika utasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa mafuta ya kula.

Aidha, Mkurugenzi huyo alisema pamoja na maeneo hayo kuainishwa lakini wawekezaji watakaojitokeza kuwekeza katika kilimo cha alizeti wanapaswa kupima afya ya udongo katika maeneo hayo.

Naye Mtafiti Mwandamizi kutoka Kituo cha TARI Ilonga kilichoko wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Ismail Ngolinda, alisema kutokana na upungufu wa mafuta ya kula nchini, wameamua kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti kwa madaraja tofauti tofauti.

Ngolinda alisema Ilonga ndiyo watafiti wa mbegu za alizeti na kwamba wamebaini mahitaji ya mafuta nchini ni tani 570,000 kwa mwaka, huku uzalishaji ukiwa ni wastani wa tani 352,908.

Alisema endapo uwekezaji wa kilimo hicho utaongezeka utasaidia kupunguza gharama za uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Naye Mkurugenzi wa Uhawilishaji wa Teknolojia na Mahusiano wa TARI, Juliana Andagile, alisema pamoja na kuonyesha teknolojia za mbegu hizo ambazo zimefanyiwa utafiti wa kutosha kwa watafiti wa TARI watawaonyesha wafanyabishara namna kutumia mbinu bora za kilimo pamoja na njia za kutumia vidhibiti magonjwa wanapofanya uwekezaji wa kilimo hicho.




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitangaza ujio wao mpya wa kampuni ya Samsung uliojaa ofa nyingi hasa katika msimu huu wa Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba). Kulia ni Meneja wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TUICO yawataka waajiri kufuata sheria

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara,Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) Mkoa wa Pwani, Kassimu Matewele, amewakumbusha waajiri kufuata sheria, kanuni na taratibu za kazi.

Matewele alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, waliotaka kufahamu hatua zilizochukuliwa kufuatia malalamiko ya wafanyakazi wa kiwanda cha kuzalisha dawa za kuulia viluilui vya mbu kilichopo Kibaha.

Alisema waajiri wakifuata sheria za kazi itaondoa kero za wafanyakazi kwenye baadhi ya maeneo na kuwafanya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Katibu huyo alisema vitu vingi haviendi kama inavyotakiwa, kutokana na baadhi ya waajiri kutofanya kazi zao ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufuata sheria na taratibu zilizopo.

Matewele alitoa tamko hilo kutokana na wafanyakazi wa kiwanda hicho kudai mishahara ya miezi mitatu.

Katibu huyo alisema wanaendelea kuyafanyia kazi yaweze kutafutiwa ufumbuzi.

Wafanyakazi hao ambao majina yao yanahifadhiwa, walisema kwa sasa wanaona kama wametelekezwa, kwani huduma za umeme na maji zimekatwa katika kiwanda, huku wakiwa wanalilia haki yao ya kutopata mishahara kwa wakati.

Walisema wanafanya kazi kwenye mazingira hatarishi ya hofu ya magonjwa ya mlipuko na pia uwapo wa wadudu wakali kutokana na eneo linalozunguka kiwanda kuzingirwa na nyasi kubwa.

## Machali awaahidi w'biashara eneo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Moses Machali, amewaahidi washiriki wa maonyesho ya Sabasaba kukaa na viongozi wa mkoa pamoja na jumuiya ya wafanyabiashara kuangalia eneo la wazi la kufanyia shughuli zao.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua Maonyesho ya 21 ya Sabasaba baada ya kukagua mabanda ya washiriki kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na nje ya nchi.

Kaulimbiu ya maonyesho hayo mwaka huu ni 'Uchumi wa Ajira na Viwanda Endelevu'.

Machali alisema eneo la viwanja vya jengo la Chama Cha Mapinduzi (CCM), linalotumiwa kwa sasa halikidhi lengo la washiriki kwa kuwa ni sehemu ndogo.

Alisema siku ya Sabasaba hailengi kuuza bidhaa pekee zinazoonyeshwa kwenye mabanda bali wapo wanaofika kwa ajili ya kuangalia na kujifunza.

Katibu Mtendaji wa Uratibu wa Maonyesho ya Sabasaba Mkoa wa Kagera (KAIDEP), Deogratius Kajua, alisema eneo la kufanyia biashara ni dogo.

Alisema kuna wafanyabiashara wengi wanaotoka nchi za Congo, Rwanda, Uganda na Kenya.

Vile vile, alisema lengo la maonyesho hayo ni kusaidia washiriki kutangaza bidhaa zao kwa kuwa mkoa huo umepakana na nchi za Afrika Mashariki ambazo baadhi yao kila mwaka hufika eneo hilo.

## Sendiga afurahishwa ujenzi wa madarasa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amefurahishwa na ujenzi wa miradi ya vyumba vya madarasa na maabara wilayani Kilolo huku akitoa muda wa wiki mbili kwa halmashauri hiyo kukamilisha miradi hiyo.

Akizungumza katika kikao cha tathmini ya ziara yake ya kukagua miradi hiyo Tarafa ya Mazombe, Sendiga alisema ameona nguvu kubwa inayofanywa na viongozi wa wilaya hiyo na ushirikiano huo unaofanywa na viongozi hao pamoja na wananchi umesukuma mbele maendeleo ya miradi hiyo.

Sendiga alisema jitihada zimeendelea kufanywa na serikali kuwakomboa watoto wa Wilaya ya Kilolo na Tanzania kwa ujumla ili wapate elimu katika mazingira yaliyoboreshwa zaidi. Alitaka kila kiongozi kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa kuwajibika katika usimamizi wa fedha za serikali na za wadau wanazochangia miradi hiyo.

Alisema miradi mingine aliyoitembelea ipo katika hatua ya umaliziaji na kuwataka viongozi wa wilaya hiyo kuongeza nguvu kuikamilisha ndani ya kipindi cha wiki mbili kuanzia jana.

Katika hatua nyingine, Sendiga alipongeza jitihada za wananchi wa Wilaya ya Kilolo uchangiaji wa miradi ya elimu na kuuagiza uongozi wa serikali za vijiji katika maeneo ya miradi ya vyumba vya madarasa na maabara kutenga siku maalumu ya kuwaonyesha wananchi shughuli zinazofanyika kupitia michango yao ili kuwatia moyo zaidi wa kuchangia miradi kama hiyo na mingine.

# W'biashara waikosha TRA utoaji risiti za EFD

**Na Christina Mwakangale**

BODI ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imesema imefurahishwa na huduma ya wafanyabiashara na kutoa risiti licha ya baadhi yao kutokuwa na mashine ya EFDs.

Imesema upo umuhimu wa kuendelea kuwaelewesha wananchi namna ya kutumia tovuti ya mamlaka hiyo, ili kufahamu pamoja na kutumia mfumo wa kubandika risiti za kielektroniki katika bidhaa.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Dk. Suleiman Missango, aliyasema hayo jana baada ya kutembelea banda la TRA kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa, Sabasaba, mkoani Dar es Salaam.

Mbali na hilo, Dk. Missango alisema mamlaka hiyo iendelee kutoa elimu ya kodi pamoja na kufahamisha umma kuhusu huduma za kimtandao ili wananchi kulipa kodi kwa urahisi.

"Nimefurahi kuona mmejiandaa vizuri kutoa elimu na huduma katika maonyesho haya. Nafahamu mnatoa sana elimu, lakini inabidi iwe endelevu, kuwafikia wananchi wengi zaidi," alisema Dk. Missango, ambaye aliongozana na baadhi ya wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Alisema kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wakurugenzi aliombatana nao huduma zinawakuwa na ufahamu wa baadhi ya huduma zinazotolewa na TRA, inabidi kutoa elimu kwa kugawa makundi mbalimbali na kuwapatia elimu.

Naibu Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Elvida Max, alisema maonyesho hayo, yanatoa fursa kwa TRA kutoa elimu kuhusu masuala ya mbalimbali na kutoa huduma ikiwamo usajili wa walipakodi na kuwapatia Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) pamoja na nyingine za kimtandao.

Aidha, katika maonyesho hayo TRA, inatoa huduma ya kusajili na kuwapatia walipakodi TIN, kutoa taarifa ya makadirio ya kodi, matumizi ya mashine za EFD bila kuwa na mashine, ubandikaji stempu za kielektroniki katika bidhaa unavyofanya kazi pamoja na maelezo ya programu za Chuo cha Kodi (ITA).



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na viongozi waandamizi wa Benki ya NBC wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Theobald Sabi (katikati), Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo, Elibariki Masuke (kulia) na Meneja Uhusiano, William Kallaghe (wapili kulia) alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Kifaa kufukuza wadudu shambani

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imegundua kifaa cha kufukuza wadudu waharibifu wa mazao shambani kinachotumia umeme wa jua.

Kifaa hicho kinajulikana kwa jina la sound birds scare, ambacho wadudu hao wanapoingia shambani huwatishia kwa sauti ya kushtua, hivyo wadudu hao hawawezi kustahimili kukaa kwenye mazao.

Akizungumza katika banda la VETA katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) mbunifu wa kifaa hicho kutoka Mikumi, Jones Hokororo, alisema walipata wazo la kutafuta suluhisho la kuwa na kifaa cha namna hiyo baada ya kusikia kilio cha wakulima kutoka mikoa mbalimbali kuhusu hasara ya mazao yao kushambuliwa na wadudu. "Tatizo la mazao kushambuliwa na wadudu ni kubwa katika mikoa mingi na wakulima wamekuwa wakilia kupata hasara kutokana na kushambuliwa na wadudu kila mwaka," alisema Hokororo.

"Wapo ambao hulazimika kuhamishia hata watoto wao mashambani hasa kipindi cha msimu wa mavuno, wanapumzika shuleni kwa kipindi fulani ili kupeana zamu ya kwenda kufukuza wadudu, kwa hiyo kupitia kifaa hiki hata watoto hawatakosa tena shuleni kwa sababu kazi hiyo inafanywa na kifaa chenyewe na wakulima hawatapata hasara tena ya mazao yao." Alisema kifaa hicho kina uwezo wa kufanya kazi hiyo saa 24 kwa kujizima chenyewe na kujiwasha na kwamba kunapokuwa na mvua hutumia betri maalum na hivyo kutoathiriwa na mvua.

"Na kifaa hiki kinapokuwa kinafukuza hao wadudu waharibifu hupiga kelele ya sauti kama ya tai au mwewe ambao hawa ndio huwa tishio kubwa kwa wadudu hao," alisema Hokororo.

"Na kwa sasa tumeruhusiwa kukipeleka sokoni ili wakulima wakinunue baada ya kupata ushindi katika Maonyesho ya Mashindano ya Kisayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka huu.

## Watanzania watakiwa kuwekeza viwandani

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wameshauriwa kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda na kwenye miradi mbalimbali, kwani serikali imewapa upendeleo maalum tofauti kwenye masuala ya kodi na tozo tofauti na wageni.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Dk. Maduhu Kazi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Alisema serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ambayo yatawawezesha Watanzania wazawa na wageni kufanya biashara katika hali ambayo haina usumbufu kama ilivyokuwa zamani.

Dk. Maduhu alisema TIC imepata maeneo manne ya kujenga viwanda vingi (Industrial Park), hivyo wawekezaji wazawa na wageni wasiwe na hofu ya kupata maeneo ya kujenga viwanda vidogo na vikubwa.

Alisema wawekezaji wengi wamekuwa na imani na mazingira mazuri ya biashara yaliyowekwa na serikali, ndiyo sababu wengi wamekuwa wakisajili miradi ya biashara na kuanzisha viwanda kwa wingi.

## Wanafunzi Mzumbe wabuni miradi ya kilimo na ufugaji

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Mzumbe wamebuni miradi mbalimbali, ikiwamo mfumo wa kisasa wa ufugaji wa samaki na wa kilimo cha mboga.

Akizungumza katika banda la chuo hicho kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, mwanafunzi mbunifu wa Shahada ya Sayansi ya Uzamili katika Mipango na Menejimenti ya Miradi tawi la Morogoro, Nelson Kisanga, alisema lengo ni kukabiliana na changamoto ya ajira.

Kisanga alisema katika kuendesha mfumo huo wa kisasa wa ufugaji, hutumia pia kubadilisha taka kuwa malighafi kwa ajili ya chakula cha samaki hao wanaowafuga.

Mhadhiri wa Chuo hicho tawi la Morogoro, Dk. Bahati Ilembo, alisema kuwa vijana 50 ambao wameendelezwa kutokana na kazi zao za kibunifu, kati yao 20 wanajitegemea kwa kutengeneza bidhaa zao na kuuza.

Rais anayesafiri ndani ya kanuni aliyoirithi, utawala bora na haki

Ukurasa 12





Ukurasa 13

**Katiba mpya maji uliyoyavulia, inakuwa vigumu kuyakimbia**



Ukurasa 14

**HELLEN AUMA WANDERA:**

**Ukitaka kuudhi anayekuudhi yadharau maudhi yake**

siasa

JUMATANO JULAI 7, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

## SIKU 100 ZA UONGOZI WAKE...

# Rais Samia katika vitendo zaidi vinavyoushikilia umoja kitaifa

**Na Mwandishi Maalum**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na maaskofu Katoliki Tanzania, Kurasini jijini Dar es Salaam, siku chache zilizopita alitoa kauli iliyowafurahisha wengi.

Alipokuwa anasikiliza maoni ya maaskofu hao, kuna jambo liliogusiwa kuhusu Zanzibar, naye akalipa ufafanuzi 'atalimaliza kinyumbani' na Askofu wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Mhashamu Augustine Shao.

Askofu Shao ni mzaliwa wa mkoani Kilimanjaro na kwa zaidi ya miaka 25 sasa, amekuwa akifanya kazi visiwani Zanzibar. Ni katika mazingira hayo, Wazanzibari (akiwamo Rais Samia) wanamwona ni mwenzao katika ujenzi wa nchi na hasa upande huo wa muungano.

Tayari kuna ahadi iliyoonyeshwa na Rais Samia ya kuwakutanisha Watanzania wote, bila ya kujali mwelekeo wao kisiasa, jambo linaloonekana kuwafurahisha wengi.

Ni hali inayodhihirishwa na matendo yake kutimiza ahadi alizotoa kuwa na serikali shirikishi, ambayo kwa Watanzania wote katika mustakabali hata mmoja anapokuwa yuko katika chama cha upinzani, pia anapewa fursa ya kutoa uamuzi mzito nchini.

Alipohutubia Bunge kwa mara ya kwanza Aprili mwaka huu baada ya kukabidhiwa madaraka ya kuongoza nchi kwa nafasi ya juu, Rais Samia alieleza kujitoa katika mipango ya kuziba pengo kati ya serikali na vyama vya upinzani, pia kutetea demokrasia na uhuru wa kimsingi.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya, ambaye ni Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga, walipokutana kwenye mkutano ukumbi wa TEC, Kurasini jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**SURA YA UTEUZI**

Rais Samia alihidi kuteua watu katika nafasi mbalimbali za serikali, pamoja na kutafuta viongozi wenye uwezo, bila kuishia katika chama tawala- Chama Cha Mapinduzi (CCM) pekee, pia kutoka vyama vya upinzani.

Ahadi ya aina hiyo iliyoanzia sura ya ndoto na ikawa katika sura ya udhahiri zaidi, katika moja ya uteuzi wake mpya hivi karibuni, hasa alipozungumza baada ya kumteua Queen Sendiga, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, aliyechukua nafasi ya Ally Hapi, aliyehamishiwa mkoani Mara.

Kisiasa, Queen alikuwa mwanachama wa CCM hadi mwaka 2014, alipojiengua na kujiunga na Alliance for Democratic Change (ADC), moja ya vyama vidogo vya upinzani nchini Tanzania. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, aligombea ubunge Jimbo la Kawe, kwa tiketi ya chama hicho, lakini hakufanikiwa.

Mwanamama huyo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa ADC, hakukata tamaa. Katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa 2020, aliteuliwa na chama chake kugombea urais nchini, akiwa miongoni mwa wanawake wawili waliojitokeza kitaifa. Mwingine ni Cecilia Mwanga wa Chama cha Demokrasia Makini.

Katika kutetea uhuru na demokrasia, Rais Samia pia aliahidi kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa upinzani, ili nao waweze kufanya shughuli zao kisiasa kwa faida ya nchi.

"Demokrasia, uhuru wa mtu binafsi na uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu kukuza maendeleo na amani. Kwa nia ya kulinda demokrasia, nina nia ya kukutana na viongozi wote wa vyama vya siasa kujadili jinsi wanavyoweza kufanya shughuli zao za kisiasa kwa faida ya nchi yetu," alisema.

Katika hotuba yake kwa taifa kupitia Bunge, vilevile Rais aliahidi kulinda uhuru wa watu na vile vile vyombo vya habari, akisisitiza uhuru na demokrasia ndio msingi wa amani kitaifa, ambayo pia inachochea maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Rais Samia alikumbusha kwamba hakuna uhuru wa kidemokrasia, ambao haujalindwa na kutawaliwa na sheria, taratibu na kanuni stahiki.

**SURA YA UTHABITI**

Pamoja na demokrasia na uhuru wa watu, Rais Samia aliwataka Watanzania kuwa thabiti katika shughuli zao kulingana na vifungu vya sheria vilivyopo nchini.

Mara tu baada ya hotuba hiyo ya rais, kambi ya upinzani ilielezea utayari wake kukutana naye na hasa kiongozi wao, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), zikifafanua kupokea barua ya Ikulu kuwaalika kwenye mkutano.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliandika kwenye mtandao wake wa 'Twitter' wa Aprili 20 mwaka huu, kwamba walishapokea barua ya majibu ya mwenyekiti wao kitaifa kutokana na ombi la kukutana na rais, hali kadhalika Rais alikubali kufanya mashauriano nao na walikuwa wanasubiri tarehe ya mkutano.

Ingawa Katibu Mkuu wa Civic United Front (CUF) Haroub Shamsi, alinukuliwa akisema hajapokea barua ya mwaliko huo mkuu, huku katika sura ya pili kukiwapo taarifa kwamba, alikuwamo katika orodha ya viongozi wa Baraza la Vyama vya Siasa Kambi ya Upinzani, waliowasiliana na mamlaka kuu hiyo ya nchi.

Kimsingi, mtazamo wa jumla wa Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa na Rais Samia, unabeba mjadala unaobeba mustakabali wa wa mwelekeo wa nchi.

INAENDELEA UK.14

SIKU 100 ZA RAIS SAMIA IKULU



SAMIA SULUHU HASSAN:

# Rais anayesafiri ndani ya kanuni aliyoirithi, utawala bora na haki

• Jicho, uamuzi wake uko ofisini, mitaani • Maudhui ya Magufuli yenye vionjo vipya



Wananchi wa Mtongani na Kwa Azizi Ali, Dar es Salaam, walipomsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akikagua ujenzi wa Mradi wa Mwendokasi, katika barabara ya Kilwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na MWANDISHI MAALUM**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ndani ya safari ya siku 100 kujumlisha ziada ya siku kadhaa sasa tangu kushika nafasi yake, amebaki kiongozi anayefuatilia sana taarifa za habari iwe redioni au runinga, magazetini na kwenye mitandao ya kijamii.

Mfano hai ni mkasa wa Stendi Kuu ya Msamvu mjini Morogoro, ambayo runinga mojawapo ilionyesha jinsi namna mama huyo alikuwa ananyanyasika na jinsi viongozi wa Manispaa ya Morogoro na namna ambavyo hakujaliwa, katika mandhari ya wafanyabiashara wadogo.

Rais Samia aliliona tukio hilo alipokuwa mkoani Mwanza na mara moja akachukua hatua, kwani hakufurahishwa na jinsi suala hilo lilivyoshughulikiwa. Hapo alibatilisha, uteuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Sheila Lukuba.

Ni uamuzi aliyoufikia alipokuwa kwenye mkutano na vijana katika mkoa wa Mwanza. Alieleza kukasirishwa na uonevu dhidi ya wafanyabiashara ndogo na mali zao kuharibiwa na serikali za mitaa, ambalo ndiyo msimamizi mkuu wa wananchi waliko mtaani.

"Juzi niliona wanamgambo wa Morogoro wakiwapiga wafanyabiashara ndogo na kuharibu mali zao. Nilihuzunika sana. Ninabatilisha uteuzi wa 'DC' na 'DED.'

"Kwa kuwa, kulikuwapo njia nyingine ambazo zingetumika kuwasiliana na wafanyabiashara ndogondogo kwa uhamishaji salama. Nilimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kushughulikia hili," alisisitiza.

Tangu kuchukua ofisi Rais Samia amekuwa wazi dhidi ya nyendo za ufisadi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya ofisi za umma, akisisitiza kuwa kila kitu kiko chini ya uangalizi salama.

> "Kwa kuwa, kulikuwapo njia nyingine ambazo zingetumika kuwasiliana na wafanyabiashara ndogondogo kwa uhamishaji salama. Nilimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kushughulikia hili.



Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kariakoo, Dar es Salaam, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kusikia na kutatua kero zao.

Anawaambia wote wanaochukulia kirahisi Serikali ya Awamu ya Sita, ni lazima wajipange kwa hatua kali za kisheria na za kinidhamu, akisisitiza kwamba haitavumilia kamwe vitendo vibaya katika ofisi za umma.

"Hatuwezi kwa njia yoyote kurudishwa kwenye siku za zamani za giza," alionya Rais Samia, huku akituma ujumbe mzito kwa viongozi wa ofisi za umma na washirika wao.

**AIDUMISHA AWAMU YA 5**

Rais Samia aliwaambia wanaofikiria kuwa vita dhidi ya rushwa viliisha kwenye kifo cha mtangulizi wake, Dk. John Magufuli, wanajidanganya kwa sababu serikali ya awamu yake inaendeleza vita ilivyorithi dhidi ya ufisadi.

Alisema, serikali itadumisha maono na falsafa ya serikali ya awamu ya tano, katika kukomesha ufisadi, kuboresha ukusanyaji mapato na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato.

Msisitizo wake ni kwamba serikali iliyopo madarakani itaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya watakaopatikana na hatia ya kutumia vibaya pesa za umma, matumizi mabaya ya ofisi na vitendo vya rushwa, ambavyo vinaanguka katika usaliti juhudi za maendeleo ya nchi.

Wakati wa siku 100 za kwanza ofisini, Rais Samia alitoa uamuzi uliolenga kulinda maslahi ya taifa na amekuwa akilifanya hilo kila wakati inavyolazimika.

Rais Samia, katika mfumo wake wa utawala, hakusita kuchukua hatua kali na za kinidhamu kwa maofisa wa umma wanaoangukia kashfa ya kutumia vibaya nafasi zao.

**RIPOTI ZA CAG**

Wakati akipokea Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mwishoni mwa Machi, Rais Samia alimsimamisha kazi Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kupisha uchunguzi, baada ya kuhusishwa na kashfa ya matumizi mabaya ya ofisi.

Ni hatua iliyoanzia kwa kuiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza suala hilo haraka, ikiwamo ukaguzi maalum wa pesa zote zilizotolewa kwa miradi ya maendeleo kati ya Januari na Machi, mwaka huu.

"Tunataka kuona ukaguzi wa fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Januari hadi Machi, mwaka huu," aliuagiza uongozi mkuu wa juu wa TRA na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

"Sasa naamuru kusimamishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa TPA ili kufungua njia ya uchunguzi wa ubadhirifu huo," alitamka.

Mkurugenzi Mkuu mteule wa sasa TPA, ni Erick Hamisi, ambaye mkuu wa nchi alimpa miezi sita kuboresha utendaji na kudhibiti ubadhirifu katika mamlaka hiyo.

Ni mwendelezo wa kichojiri Desemba mwaka jana, pale Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipowasimamisha kazi maofisa wawili wa TPA watokao Idara ya Fedha, kwa tuhuma za ubadhirifu wa pesa za umma. Pia ndani ya historia kama hiyo, Rais Samia alimsimamisha kazi Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, ambaye sasa ana kesi mahakamani.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais wa wakati huo, Gerson Msigwa, haikutoa maelezo zaidi, lakini badala yake ilisema uamuzi wa rais ulikuwa utekelezwe mara moja.

**ZIARA YA GHAFLA**

Mapema mwezi uliopita, Rais Samia alifanya ziara ya ghafla katika Soko la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, baada ya kupata shaka na mwenendo wa usimamizi wake na aliwasimamisha viongozi wa Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC), alipohisi kuwapo kasoro kubwa za uendeshaji wa kituo kikubwa cha ununuzi nchini.

Mkuu huyo wa nchi, aliamuru vyombo vya usalama kufanyika uchunguzi juu ya hali ilivyo katika sokoni hilo linalohudumia nchini na mataifa jirani, kwa hatua zaidi.

"Nimepata wasiwasi na nimeamua kutembelea soko ili kujionea mwenyewe shida zinazowakabili wafanyabiashara, kwa kuzingatia kwamba Kariakoo inakusanya sehemu kubwa ya biashara zote zinazofanywa nchini.

"Baada ya kuzunguka na kuzungumza na baadhi yenu, nilipata picha wazi ya jinsi mambo yanavyoendeshwa hapa na sikufurahishwa na hali hiyo hata kidogo," aliongeza.

Daima, ni hatua inayoangukia tafsiri ya awali ya serikali ya sasa kuendeleza hatua za zama za marehemu Rais Dk. Magufuli, kuhakikisha inawasaidia wafanyabiashara ndogo, kuwa katika mazingira rafiki.

Ni tafsiri pana inayoangukia simulizi za mwendelezo kutambua shughuli za wafanyabiashara ndogo, kupitia utoaji wa vitambulisho.

# Katiba mpya maji uliyoyavulia, inakuwa vigumu kuyakimbia

**Na Sabato Kasika**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametangaza msimamo wa awamu yake kuwa haina mpango wa kuingia kwenye mchakato wa katiba mpya na kwamba kipaumbele chake ni kujenga na kuimarisha uchumi, kupata wawekezaji na kuboresha maisha ya Watanzania.

Kuwekwa kando suala la kuandikwa katiba mpya pamoja na mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa ni msimamo unaoibua mjadala kutoka kwa wadau mbalimbali katika mitandao ya kijamii licha ya kwamba Rais anawaomba wananchi wamuunge mkono katika harakati za kufufua uchumi, na pia anawataka wanasiasa kuwa na subira kuhusu mchakato wa katiba mpya na mikutano ya hadhara ya kisiasa.

"Kwa sasa tumeruhusu mikutano ya ndani ya siasa, wabunge kwenye maeneo yao, lakini siyo mbunge atoke eneo lake aende kwingine, lakini ile ya hadhara, tujipe muda." Anaongeza: "Mchakato wa katiba mpya, sisemi katiba si ya maana, hapana, nipeni muda kwanza tujipange kiuchumi". Ndivyo anavyosema alipokutana na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam.

Msimamo huo ndiyo unaozusha mjadala kwenye mitandao ya kijamii ukihusisha wanasiasa wa vyama vya upinzani na hata wa CCM wakiwamo ambao wanakubaliana naye huku wengine wakipingana na maelezo ya kusubiri kwanza .

Kwa mfano, Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Shinyanga, unasema unamuunga mkono Rais Samia kuwa haukubaliani na wazo la kuanzishwa kwa mchakato wa katiba mpya.

Mwenyekiti wa UVCCM wa mkoa Baraka Shemahonge, ndiye anayesema hayo wakati akizindua shina la wakereketwa tawi la Negezi pamoja na ufunguzi wa ofisi.

Shemahonge anasema, chama hicho hakina ajenda, wala wazo la kuanzisha mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya, bali kina kazi kubwa ya kujenga nchi na kuwaletea maendeleo Watanzania.

"Tunamuunga mkono Rais wetu Samia kwa kukataa mchakato wa katiba mpya, kwani nchi ipo katika vita ya kuinuka kiuchumi, inapambana na janga la corona na siyo katiba mpya," anasema.

Pamoja na Shinyanga vijana wa Manyara wanasisitiza umuhimu wa kubaki na katiba iliyopo kwa maelezo kuwa taifa limefikisha zaidi ya miaka ya 50 likiongozwa na katiba iliyopo sasa.

Mwenyekiti wa UVCCM wa mkoa huo, Francis Komba anasema, kama isingekuwa katiba bora yangeweza kutokea mambo mkanganyiko na kwamba anashangaa kusikia watu wakiwa na mashaka na katiba ambayo imelinda wa Watanzania, maendeleo yao kiuchumi, kisiasa na kijamii.

"Katiba yetu inatoa majibu katika kila swali gumu. Imezingatia matakwa ya utawala, demokrasia, haki, sheria na hata nyakati ngumu za kubadilishana madaraka," anasema Komba.




Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ambaye anasema suala la kuwapo Katiba mpya ni la msingi. **PICHA: MTANDAO**

### HITAJI LA WOTE

Mjumbe wa Bodi ya Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, anasema katiba mpya ni hitaji la Watanzania wote, lakini anaamini uwezekano wa kuwapo katiba hiyo kwa sasa ni mdogo.

"Ninaamini kwamba kazi kubwa ya Rais Samia kwa sasa ni kuhakikisha CCM inashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na ukumbuke kuwa katiba mpya haiwezi kusaidia CCM kushinda," anasema Mwakagenda.

Hata hivyo, anafafanua kuwa kutokuwapo kwa mchakato wa katiba mpya kunaweza kukwamisha hitaji hilo la Watanzania, ambapo anashauri kuwa pamoja na Rais kuimarisha uchumi, angehakikisha inapatikana haraka.

"Rais anakiri kwamba, katiba mpya ni ya muhimu na anataka apewe muda ili kuimarisha uchumi wa nchi, hilo ni jambo jema, kwa sababu mchakato wa katiba unahitaji fedha, lakini hatua hiyo isichukue muda mrefu," anasema.

Mwakagenda ambaye ni mchambuzi wa siasa, anasema, katiba ya sasa imepitwa na wakati, na kwamba ndiyo maana watu wengi wamekuwa wakitamani kuwapo mpya inayoendana na mazingira ya sasa.

### NI SAWA LAKINI...

Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe, anasema katika kipindi kifupi ambacho Rais Samia ameingia madarakani, kuna mabadiliko makubwa ameyaona hasa kutobughudhiwa kwa viongozi wa chama hicho.

Hata hivyo, anasema, suala la kuwapo kwa katiba mpya ni la msingi, hivyo anatamani ahadi ya Rais ya kukutana na viongozi wa chama hicho itimie, na kwamba wao kama viongozi wa chama kikuu cha upinzani wana mengi

"Ni muhimu viongozi wa chama chetu kukutana na Rais, kwani yapo mengi ambayo tunatamani kujadili naye kwa mustakabali wa taifa likiwamo la kuwapo katiba mpya isiyo na viraka," anasema Mbowe.

Anasema, anaamini kuwa Rais ameweza kuzuia kukamatwa kwa viongozi na wanachama wa upinzani na kwamba hata kwenye suala la kuibua mchakato wa katiba mpya akiamua anaweza.

"Rais anaendelea kukutana na makundi mbalimbali, nasi tunaimani kukutana nayo, lakini siyo kwamba tunampangia, bali yeye mwenyewe ataangalia ni lini ana nafasi ili atuite tukazungumze naye.

### WATU WANAPOAMUA

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema Rais ameshusha pumzi za Watanzania na hali ya hofu na sintofahamu iliyokuwa imetanda nchini imeondoka.

"Ameonyesha anavyojiamini na kusimamia haki, hivyo ningemshauri ajitahidi kwenye suala la sheria mama ambayo ni katiba, aanzishe mchakato haraka ingawa anataka kuimarisha uchumi kwanza," anasema Dk. Kijo-Bisimba.

Dk. Kijo-Bisimba pia anamshauri Rais kuwa macho na wanaomzunguka wasimsifie tu, kwa madai kwamba wanaweza kuyumbisha msimamo thabiti alionao ambao wakati mwingine unaweza kuharibiwa na wapambe.

"Lakini kuna mambo ambayo angeweza kuyafanya, lakini bado, hasa kukutana na wapinzani wa serikali yake ambao wanaonekana wana maumivu na wangependa kuhakikishiwa uhuru wao kuendesha siasa," anasema.

Anasema, pamoja na kutamani kuwapo kwa mchakato wa katiba mpya, anatamani pia kuona Rais akikutana na wapinzani, ambao wanaonekana kuwa na maumivu na wangependa kuhakikishiwa uhuru wao kuendesha siasa.

" Ameonyesha anavyojiamini na kusimamia haki, hivyo ningemshauri ajitahidi kwenye suala la sheria mama ambayo ni katiba, aanzishe mchakato haraka ingawa anataka kuimarisha uchumi kwanza.

### ULIKOTOKEA

Mchakato wa katiba mpya ulianza wakati wa serikali ya awamu ya nne baada ya Rais wa wakati huo, Jakaya Kikwete kuelezea nia ya serikali yake ya kuanzisha mchakato huo.

Hatua hiyo ilifuatiwa na kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83/2011 na baadaye ikatungwa nyingine ya Kura ya Maoni Na. 11/2013, na kuundwa Tume ya Jaji Joseph Warioba, iliyoratibu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na kuandaa rasimu ya kwanza ya katiba.

Rasimu hiyo ambayo ilihaririwa na mabaraza ya katiba na kupatikana rasimu ya pili ya katiba, ambayo ilipelekwa kwenye Bunge Maalum la Katiba (BMK) na Rais Samia alikuwa Makamu Mweyekiti wa bunge hilo ambalo lilikuwa na mivutano mingi hadi kusababisha wajumbe kutoka upinzani kususia.

Licha ya upinzani kususia bunge hilo, vikao viliendelea hadi ikapatikana katiba inayopendekezwa, lakini baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakidai kwamba, haina muafaka na maridhiano ambayo ndiyo msingi wa kupata katiba bora ya kitaifa yenye kukubalika na wengi.

Kutokana na hali hiyo, mara tu baada ya Rais Samia kuingia madarakani Machi mwaka huu, wapinzania waliomba suala la mchakato wa kupatikana katiba mpya liwe mojawapo ya mambo anayoyapa kipaumbele.

JUKWAA LA UONGOZI

HELLEN AUMA WANDERA:

# Ukitaka kuudhi anayekuudhi yadharau maudhi yake

• Aliitwa anayenuka shombo leo kawa mbunge

Na Christina Mwakangale

HELLEN Auma Wandera, ni miongoni mwa wanawake waliotimiza ndoto ya kuwa viongozi wakiwa na umri mdogo tena, licha ya kupitia misukosuko mingi ikiwamo kutukanwa kuwa ananuka shombo.

Hellen mwenye miaka 23 ni mbunge, mwakilishi wa Jimbo la Busia, nchini Uganda ambaye maisha yake yamejaa simulizi za kusisimua, mafunzo na hata kutoa ushawishi kwa wasichana wenye matarajio makubwa wanaoishi kwenye hali ngumu kuiga alivyofanikiwa na kuwa kiongozi na mtu anayejitegemea.

Tangu mwanzo alikuwa mjasiriamali tena msichana ambaye hakuhofia kuchekwa na jamii huku baadhi wakimwambia ananuka harufu ya shombo ya samaki, aliowauza ili kujipatia riziki na kumudu maisha yake.

Ni mbunge mdogo zaidi katika bunge la Uganda, mhitimu wa elimu ya juu, alishinda kiti cha ubunge kupitia chama kinachotawala cha NRM wilayani Busia, mashariki mwa nchi hiyo katika uchaguzi wa Januari mwaka huu. Anasimulia safari yake hadi aliposhinda uchaguzi na kuwa mbunge ambaye anatarajia kufanya makubwa kwa familia na wapigakura wake.

### SIMULIZI MAISHANI

Akiwa amebandikwa jina la Mama Busia ni Mbunge wa Viti Maalum Wilaya ya Busia, jimbo lililo jirani na mpaka wa Kenya. Ana historia ndefu hadi kuchaguliwa kwake na wananchi kuwa mbunge akiwa amehitimu masomo katika Chuo Kikuu cha Kyambogo mwaka 2019 na kupata shahada ya sayansi ya jamii.

Akiwa masomoni Kampala alikuwa akifanya biashara ndogo ndogo, ili kujikimu kimaisha. Akinunua samaki na kuwaandaa kisha kuwafunganya na kuwauzia wanafunzi wenzake chuoni, na anasema alifanya hivyo kutokana na pesa alizokuwa anapewa hazikutosha kujikimu.

Hellen anasema baba yake ni mwalimu wa shule ya msingi na mama yake ni muuza samaki, kazi aliyoirithi na iliyomfanikisha akatoka kimasomo na sasa ni mbunge. Kwa maelezo ya Hellen, mama yake alianza biashara ya kuuza samaki katika soko la Banda kitongoji kilichopo jijini Kampala .

"Nilibeba samaki katika mfuko wa plastiki nikiwapelekea wateja, lakini wasichana wenzagu chuoni walinicheka nikawauliza nani bora mimi ninayenuka samaki au ninyi mnauza miili yenu usiku?"

Hellen anasema aliwapuuzia mbali, akadharau kuchekwa na wanafunzi wenzake na akaendelea kufanya biashara ya kuuza samaki hadi mwaka jana, alipoanza kampeni kwa ajili ya kugombea kiti cha ubunge wilaya ya Busia kupitia chama tawala cha NRM.



Hellen katika harakati za kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

> Kampeni za kugombea kiti cha ubunge nchini Uganda huhitaji fedha nyingi kuwashawishi wapigakura.

### ALIVYOPITIA USHINDI

Hellen anaelezea jinsi alivyoanza kampeni zake na kupata matatizo na kubadili kuwa changamoto akisema: "Mimi nilikuwa msichana mdogo nimehitimu chuo kikuu, sijaolewa na mara nyingi kiti hicho ni kwa mwanamke aliyeolewa hivyo wengi walinidharau, lakini haikunikatisha tamaa baada ya mwezi mmoja nilijulikana jimboni nikiwa mmoja wa wagombea watatu waliokuwa juu, ndipo nikaanza polepole".

"Kampeni za kugombea kiti cha ubunge nchini Uganda huhitaji fedha nyingi kuwashawishi wapigakura. Ilikuwa ni changamoto na fursa ya kuwa mbunifu na kulazimika kutumia baiskeli kuwafikia wapigakura nikiwa mikono mitupu."

Anasema: "Kuwakusanya watu na kuwapa Shilingi 20,000 au 30,000 waliona kama mzaha baadhi yao walinitukana nikawajibu mnataka niibe. Mimi sina fedha. Mama mmoja aliniambia unazungumza vizuri lakini wewe mwembamba sana, nikamjibu wembamba siyo ugonjwa, jina hilo likaniletea umaarufu sana sitaliacha hata nikinenepa."

### UBUNGE NA NIA

Hellen hivi sasa ni mbunge wa Busia baada ya kuapishwa miezi kadhaa iliyopita. Ni miongoni mwa wabunge 529 wa bunge la Uganda na kwamba ana nia kabambe ya kutimiza ahadi na malengo yake kwa wananchi waliomchagua.

"Kwanza nataka kusaidia familia yangu ni maskini sana, pili kushirikiana na serikali kusaidia watu wa jimbo langu la Busia, kuna dhahabu lakini Wachina wameyachukua wananchi hawafaidiki nayo," anasema Hellen na kuongeza kuwa licha ya kuwa na umri mdogo bungeni, umbo dogo, anatarajia makubwa na anatoa wito kwa vijana wenzake na hasa wanaotoka katika familia maskini kutokata tamaa kama wana malengo ya kufanya mambo fulani hata kama hawana pesa akisema fedha sio inayotatua kila changamoto au tatizo.

Anasema alionyesha nia yake na hatimaye imetimiza bila kuwa na fedha za kuwapatia wapigakura na anaungana na Proscovia Alengot Oromait kuweka historia ya kuwa wabunge wadogo katika bunge la Uganda, wakati Proscovia alichaguliwa mwaka 2011 kuwa mbunge wa Usuk, akiwa na umri wa miaka 19 Hellen ana miaka 23.

**MITANDAO**

## Rais Samia katika vitendo zaidi vinavyoushikilia umoja kitaifa

INATOKA UK.11

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, amenukuliwa kumwandikia rais kumshauri masuala manne muhimu, anayoyataja kuwa ni: Hitaji la kuboresha demokrasia ya nchi na sheria; kukuza haki za binadamu; kujenga upya uchumi uliohabiwa na ugonjwa Covid-19; na wataalamu kushiriki ukabili wa corona.

Shamis, pia amenukuliwa akisema kwamba kupitia barua hiyo, Rais pia alishauriwa juu ya njia za kupata mikopo yenye riba ndogo kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) na Reli ya Mwendo Kasi (SGR).

Katika kinachohesabiwa kama kufanyia kazi ushauri wa chama hicho cha siasa cha upinzani, ndani ya wiki tatu za kuwa madarakani, Rais aliunda kamati ya wataalamu kumshauri kuhusu hadhi ya Covid-19 nchini na hatua muhimu za kuchukua kuwaweka watu salama.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo Bara, Joram Bashange, pia ameshanukuliwa akisema chama hicho kina mengi ya kuwasilisha mbele ya mkuu wa nchi, ambaye kwa matumaini angeweza kuwapa muda wa kutosha kabla ya mkutano.

Bashangea anasema, chama hicho hakifahamu njia atakayotumia kukutana nao, iwe moja kwa moja au kupitia Baraza la Vyama vya Siasa chini ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, au taasisi zingine. Anasema, Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa pia unapaswa kujadili namna ya kurekebisha sheria tofauti, pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa nchini.

### MSAJILI VYAMA

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, ameshariportiwa kuthibitisha kwamba ofisi yake ilikuwa ikiandaa mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa linalotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Nyahoza anakanusha mkutano aina hiyo, hauna uhusiano wowote na mkutano wa Rais na Vyama vya Siasa vya Upinzani. Anafafanua: "Ni bahati tuu kwamba Rais amepanga kukutana na viongozi wakuu wa vyama vya siasa wakati ambao tulikuwa tunaandaa mkutano wa kisheria wa baraza."





# Maofisa ardhi wafundwa kutumia lugha za staha

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amewataka maofisa ardhi pindi wanapotatua migogoro ya ardhi kwa wananchi watumie kauli nzuri ili kuepuka malalamiko.

Mtaka aliyasema hayo jana jijini hapa katika mwendelezo wa kampeni ya siku 10 za kutatua migogoro ya ardhi kwa wananchi maeneo mbalimbali.

Aliwataka maofisa hao kila mmoja abebe dhamana ya kutatua kero zinazohusu ardhi kwa kutumia lugha zenye staha kwa sababu hawajui wanaowasaidia baadaye watakuwa nani siku moja.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliwasisitizia wananchi kuzitumia siku 10 zilizotengwa kupeleka malalamiko ya migogoro ya ardhi ili serikali iweze kuitatua.

"Ifike mahali suala la migogoro ya ardhi Dodoma liishe, tunaamini wataalamu wa ardhi kazi hii mtaifanya kwa uaminifu na mtawapatia wananchi haki zao," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Alpha George alisema wanaamini matatizo yao yatashughulikiwa vizuri na kulifanya jiji hilo wananchi wake kuishi bila migogoro inayohusu ardhi.

Regina Bilingi mkazi wa Makulu alisema walikuwa na mashamba eneo la Tambukareli ambayo kwa sasa ni Medeli lakini bado hawajapewa fidia.

"Tunaomba serikali itusaidie katika hili tunahitaji kupata haki zetu bila kubughudhiwa kama tulivyokubali kuachia mashamba hayo," alisema.



Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Benki ya TPB, Diana Myonga (wa pili kulia), akijiandaa kukata utepe kuzindua majengo ya vyoo yenye thamani ya Sh. milioni 56.2, yaliyojengwa na benki hiyo, katika Shule ya Msingi Ifwagi, wilayani Mufindi, mkoani Iringa juzi. Katikati ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Imani Nyoni na (wapili kushoto) ni Kaimu Meneja Mwandamizi wa Mawasiliano na Uhusiano wa benki hiyo, Chichi Banda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Viongozi wa dini acheni kugawa waumini kwa siasa'

**Na Peter Mkwavila,** MTERA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Pentekoste Tanzania, Anyimike Mwakalasya, amekemea baadhi ya viongozi wa dini wanaojiingiza kwenye siasa na kusababisha kuwagawa waumini wao.

Kiongozi huyo wa dini alitoa kauli hiyo jana wakati wa mafunzo yaliyohudhuriwa na viongozi wa dini na siasa yaliyofanyika kwenye kanisa la PHAM (T) Mtera wilayani Mpwapwa.

Alisema viongozi wa dini ambao wameitwa kwa ajili ya kumtumikia Mungu hawapaswi kujihusisha na vyama vya siasa kwa kuwa watawagawa waumini.

Mwakalasya alisema hivi sasa wapo baadhi ya viongozi wa dini ambao wamejichanganya kwenye siasa na kusahau wito wao walioitiwa wa kumtumikia Mungu na wamejikuta wakitoa kauli zinazo wachanganya waumini wao.

"Tunapaswa kuwahamasisha Watanzania kuiombea nchi, ufanyaji wa kazi kwa bidii, kukemea maovu na hata kwa watumishi wa serikalini waliopewa madaraka wanaokwenda kinyume na katiba ya nchi.

"Baadhi ya viongozi wa dini wamejificha kwenye vyama vya siasa na wamesahau wajibu wao kama watumishi wa Mungu walioitwa kwa ajili ya kuwaombea hao wanasiasa pamoja na taifa ambalo Mungu ametoa jukumu kubwa kwetu."

Aliwataka viongozi wa umoja wa madhehebu ya dini kuhakikisha wanawahamasisha waumini wao kwenye nyumba za ibada kuliombea taifa.

Askofu mstaafu wa Kanisa la PHAM (T) Mtera Staaf Aswile Mwandambo, aliwashauri viongozi wa madhehebu ya dini kuwa na utaratibu ambao utakaowezesha kufanyika kwa maombi ya mnyororo kwa kupitia makanisa kwa kuishirikisha serikali.

# Ndejembi akabidhi saruji kutatua tatizo elimu, afya

**Na Ibrahim Joseph,** CHAMWINO

MBUNGE wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi, amekabidhi msaada wa mifuko ya saruji 1,136 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule na taasisi za afya.

Msaada huo aliukabidhi jimboni humo mwishoni mwa wiki iliyopita kupitia hafla fupi ambayo ilihudhuriwa na baadhi ya viongozi na wawakilishi wa wananchi.

Ndejembi aliwataka watendaji wa Serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kusimamia saruji hiyo itumike kwa malengo yaliyokusudiwa ili kupunguza matatizo kwenye maeneo yaliyolengwa.

"Msaada huu utasaidia ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Mapinduzi ambayo itapatiwa mifuko 150, Shule ya Sekondari ya Msanga mifuko 150, Shule ya Msingi Manyemba, Shule ya Msingi Ikombo, ujenzi wa choo shule ya msingi Gwandi na nyumba ya mwalimu katika Shule ya Msingi Mlimwa.

Shule nyingine za msingi ni Magungu Kimeji na Mahata Shikizi ya Itiso. Tutajenga nyumba ya mganga wa afya wa Chenene na Makoja."

Mbunge huyo aliahidi kuongeza mifuko zaidi kwa idadi hiyo hiyo kabla ya mwaka huu kuisha kwa ajili ya maeneo mengine ambayo hayajapata mgawo huo.

Pia aliahidi kusaidia serikali katika kupunguza tatizo la miundombinu ya barabara zilizoharibika kwenye maeneo mengi jimboni humo.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wenzake, Mtendaji wa Kijiji cha Kimeji, Lista Nzeje, watasimamia msaada huo ili ukatumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ofisa Tarafa wa Chamwino, Mohamed Mfaki, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, msaada huo utapunguza matatizo kwenye maeneo hayo.





# Samia aungwa mkono utunzaji wa mazingira

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JUMLA ya mitungi 500 ya gesi ya kupikia inatolewa kwa wanawake 500 wa Mkoa wa Mbeya, lengo kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kuhamasisha utunzaji wa vyanzo vya maji.

Katika hotuba yake Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wanawake jijini Dodoma, alisema miongoni mwa masuala anayopenda kuona yakishughulikiwa ni utunzaji wa mazingira.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliamua kumuunga mkono Rais Samia kwa kuanzisha kampeni ya utunzaji wa mazingira kwa kutoa elimu kwa wanawake wa Mkoa wa Mbeya na kuwapatia mitungi ya gesi ili waendelee kuwa mabalozi kwa wengine.

Akizungumza jana wakati wa kupokea mitungi hiyo kutoka kwenye kampuni ya Oryx, Mahundi alisema licha ya kuunga mkono dhamira ya Rais Samia katika utunzaji wa mazingira nchini, lakini ni sehemu ya kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mbeya kumchagua kuwa mbunge wa wanawake.

Alisema mitungi hiyo itawasaidia wanawake kuondokana na matumizi ya kuni pamoja na mkaa badala yake wanatumia nishati mbadala ya gesi, ambayo husaidia kuokoa gharama na muda.

"Nimekuja kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mbeya kwa kunichagua kuwa mbunge wao, nimeona nisiwashukuru mikono mitupu, nimewaletea mitungi 500 ya gesi ambayo itagawiwa kwa wanawake 500 vigezo na masharti vilishapatikana wasaidizi wangu watabeba jukumu hilo, nawahakikishia wanawake wenzangu kupitia kampeni hii," alisema.

Alisema mategemeo yake ni kuona Mkoa wa Mbeya unakuwa ni balozi wa kuokoa mazingira, na kwamba mwanamke nawe kinara katika eneo hilo kwa kuhakikisha wanatunza vyanzo vya maji na misitu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Gesi ya Oryx Tanzania, Araman Benoit, alisema alifurahishwa na wazo la Mahundi juu ya kampeni ya utunzaji wa mazingira mkoani Mbeya.

Alisema kutokana na kampeni hiyo, waliamua kumuunga mkono kwa kumpatia mitungi 500 ya gesi ili kuwagawia wanawake wa Mkoa wa Mbeya, ambao watakuwa mabalozi wa kuokoa mazingira na kutunza vyanzo vya maji kuzunguka maeneo yao.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (katikati), akipokea mitungi 500 ya gesi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Oryx, Araman Benoit (kushoto), jijini Mbeya jana, kwa ajili ya kuwapatia wanawake 500 ili kuwawezesha kukabiliana na uharibifu wa mazingira. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wazazi waaswa dhana potofu chanjo za watoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZAZI mkoani Mbeya wameaswa kuachana na dhana potofu kwamba chanjo zinazotolewa kwa mabinti wenye miaka 14 shuleni zina madhara kiafya.

Badala yake watambue chanjo hizo zinawalinda mabinti kuepukana na saratani ya mlango wa kizazi.

Wito huo ulitolewa juzi na Mratibu wa Huduma za Chanjo Mkoa wa Mbeya, Dk. Danford Barnabas, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mwitikio wa mabinti kupata chanjo ya satarani ya mlango wa kizazi.

Alisema kumekuwa na dhana potofu kwa baadhi ya wazazi kuwakataza mabinti zao wasipate chanjo kwa madai kuwa zinalengo la kuwadhuru kiafya.

Alisema dhana hiyo sio ya kweli badala yake binti wa miaka 14 ni muhimu kupata dozi mbili kila baaada ya miezi sita, ili kuepukana na saratani ya mlango wa kizazi ambayo imekuwa tishio nchini.

"Mwitikio kwa mabinti kupata chanjo ya kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi sio mkubwa sana, kutokana na wazazi kuwakatalia wasipate chanjo hiyo... tunaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wake pamoja na kuwaonyesha madhara kwa binti akikosa chanjo hilo," alisema Dk. Barnabas.

Alisema asilimia 40 ya wanawake nchini wanaugua saratani ya mlango wa kizazi, na kwamba ili kuzuia ugonjwa huo ni muhimu binti wa miaka 14 akapatiwa chanjo.

Daktari wa Saratani Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Magdalena Manjano, alisema miongoni mwa sababu zinazochangia saratani hiyo ni mabinti kuwahi kufanya ngono wakiwa kwenye umri mdogo, ngono zembe na magonjwa ya zinaa.

Aliongeza kuwa wanaendelea kutoa huduma za uchunguzi wa saratani hiyo kwa wanawake wenye umri wa kuanzia miaka 30, umri ambao endapo mtu ana dalili za ugonjwa huo zinaanza kuonekana.

# Wataka uchunguzi wa mil. 162/- za vyoo

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WANACHAMA wa Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko, Madibira (MAMCOS) Wilaya ya Mbarali, wameomba serikali kuunda tume huru ya kiuchunguzi uhalali wa matumizi ya shilingi milioni 162 zilizochangwa na wanachama kwa ajili ya ujenzi wa vyoo 100 eneo la mradi.

Hatua ya kuhitaji kufanya uchunguzi inatokana na vyoo vilivyojengwa na chama hicho kubomoka kwa muda mfupi tangu kukamilika kwake.

Kupitia mkutano maalumu wa chama hicho waliibuka na hoja ya kutokuwa na imani na uhalali wa matumizi ya fedha hizo ambazo miongoni zilitumika kwenye ujenzi wa vyoo.

Mmoja wa wanachama hao, George Ngailo, alisema ili kubaini ukweli wa matumizi ya fedha shilingi milioni 162, ni vyema kukaundwa tume huru kuchunguza namna fedha hizo zilivyotumika.

Aliwaomba viongozi wa ushirika huo kutokuingia tume hiyo itakayoundwa ili kuupata ukweli wa nani alitafuna fedha hizo za wanachama na hatua za kisheria zichukuliwe.

Mwanachama mwingine, John Nungu, alisema viongozi wa vyama vya ushirika hawatoi majibu sahihi ni yapi matumizi ya fedha hizo na kuishia kutoa ahadi kwamba watawasomea mapato na matumizi.

Mwenyekiti wa bodi ya chama hicho, Nurdin Petwa, aliahidi kushughulikia malalamiko hayo, huku akiwaomba wanachama kuwa wavumilivu wakati utaratibu mwingine ukiendelea.

Naye Ofisa Ushirika Wilaya ya Mbarali, Amos Ndabila, alisema hatua zinazoendelea kuchukuliwa ni kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo, na kwamba watashirikiana na vyombo vingine kubaini ukweli wa tuhuma hizo ikiwamo ujenzi wa vyoo vya chama hicho chini ya kiwango.

Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za vyama vya ushirika, Mkoa wa Mbeya ilionyesha ujenzi wa vyoo hivyo ni miongoni mwa kasoro zilizosababisha chama hicho kupata hati isiyoridhisha.

Aidha kupitia mkutano huo wanachama wameitaka bodi na watendaji wake wote wa Madibira Mamcos kukaa pembeni wakati wakisubiri tume maalumu ya uchunguzi wa matumizi ya fedha hizo na mali zingine za chama kutoka serikalini.



## Waahidiwa barabara ndani ya muda mfupi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewahakikishia wananchi wa Shehiya ya Kiongwe kuwa Barabara ya Bumbwini - Kiongwe, itajengwa kwa kiwango cha lami na kukamilika katika kipindi kifupi kijacho.

Dk. Mwinyi alitoa ahadi hiyo jana alipozungumza na wananchi wa Shehiya ya Kiongwe na vijiji jirani baada ya kutembelea na kukagua matayarisho ya mradi wa Barabara ya Bumbwini hadi Kiongwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na mradi wa upelekaji umeme na majisafi na salama.

Alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 7.8, itajengwa kwa kiwango cha lami na matayarisho ya msingi ya ujenzi huo yamekamilika.

Rais Mwinyi alisema kila binadamu anahitaji maji, ikiwa sehemu ya mahitaji ya msingi ya maisha yake, hivyo akaahidi kusimamia uwekaji wa mabomba kwa wastani wa kilomita tano.

Pia, aliiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kujenga madarasa sita yanayohitajika kwa wananchi wa shehiya hiyo ili kuwawezesha wanafunzi wa shule iliyopo kijijini huko kupata huduma za elimu kwa ufanisi.

Aliwahakikishia wananchi wa shehiya hiyo kuwa serikali itatoa unafuu katika kuwaunganishia umeme, huku matayarisho ya kazi hiyo yakiwa katika hatua za mwisho kukamilika.

Rais Mwinyi pia alilitaka Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuhakikisha kijiji jirani na shehiya hiyo nacho kinapatiwa huduma za umeme ili wananchi kunufaika na huduma hiyo.

Dk. Mwinyi alikiri wavuvi wa Zanzibar wakiwamo wa Kijiji cha Kiongwe wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vifaa vya kisasa vya uvuvi, hivyo kuendelea kutumia vifaa duni na kushindwa kufikia malengo yao.

Alisema mikakati ya serikali katika kuleta mageuzi ndani ya sekta hiyo iko dhahiri na kero hiyo kwa wavuvi itashughulikiwa.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi aliwahakikishia wananchi wa Shehiya ya Donge Chechele kuwa barabara ya Donge Mbiji hadi Chechele, yenye urefu wa kilomita mbili, itajengwa kwa kiwango cha lami pamoja na kulijenga daraja lililopo ili kuwawezesha wananchi kusafirisha bidhaa zao kutoka mashambani, hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi.

Katika ziara yake hiyo, Rais Mwinyi pia aliweka jiwe la msingi la Kituo cha Afya Mbuyu Maji na kutembelea ujenzi wa shule katika Kijiji cha Matemwe Mbuyu Maji.

# Rais Mwinyi amhakikishia jambo Katibu Mkuu CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemhakikishia Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, kuwa ataendelea kushirikiana naye katika kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatekelezwa ipasavyo.

Rais Mwinyi ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, aliyasema hayo alipokutana na ujumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ulioongozwa na Katibu Mkuu Chongolo Ikulu jijini Zanzibar.

Katika mazungumzo hayo, Rais Mwinyi alitumia fursa hiyo kuwapongeza viongozi hao wakiwamo wapya pamoja na wale wa zamani kwa kuendelea kubaki katika nafasi zao na kuahidi kuendelea kushirikiana nao katika kutekeleza majukumu ya chama na serikali.

Dk. Mwinyi alisema tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, akikumbusha kuwa hivi karibuni ilipitisha bajeti ya kwanza ya serikali anayoingoza na kilichobaki ni kuhakikisha yale yote yaliyoahidiwa kwa wananchi yanatekelezwa.

Alisema watakapokuwa tayari kuuangalia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Serikali zote mbili, wawe huru kueleza yale yote yanayopaswa kufanywa vizuri zaidi kwa lengo la kuitakia mema CCM na serikali zake mbili.

Katibu Mkuu Chongolo alisema ziara yao Zanzibar kukutana na Rais Mwinyi pamoja na ujumbe wake huo ni kujitambulisha na kuzungumza na baadhi ya wanaCCM wa Zanzibar.

Alimpongeza Rais Mwinyi kwa niaba ya sekretarieti kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wa Zanzibar huku akitumia fursa hiyo kumkabidhi Azimio la Halmashauri Kuu ya Taifa la kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Wakati huo huo, Rais Dk. Mwinyi amekutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Taasisi inayoshughulikia misaada ya kibinadamu kutoka Umoja wa Nchi za Kiarabu (UAE), Sheikh Ahmad Al Nazir Al Falasi na ujumbe wake.

Katika mazungumzo yao, Rais Mwinyi ameihakikishia taasisi hiyo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kushirikiana nao katika kuimarisha huduma za kijamii na zile za kimaendeleo.

Sheikh Ahmad Al Nazir Al Falasi alisema azma ya taasisi anayoiongoza ya kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya Zanzibar inatekelezwa.

Al Falasi alisema mbali ya kuunga mkono juhudi hizo, pia amevutiwa na mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Zanzibar na kuahidi kutekeleza azma yake hiyo.



Meneja Masoko Zantel Zanzibar, Rukia Mtingwa (kushoto), akifafanua jambo kwa Ofisa Mkuu wa Fedha Zantel, Azizi Said Ali (katikati) na Mkuu wa Mauzo na Usambazaji, Emmanuel Joshua, baada ya kumalizika kwa uzinduzi wa msimu wa manunuzi ya karafuu wa mwaka 2021/2022 huko bandarini Wete juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Corona yatajwa shida katika mfumo chakula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MATATIZO ya mfumo wa chakula yamechangiwa na uwapo wa janga la corona ambalo limeathiri upatikanaji wa chakula kwa jamii hasa zile ambazo zinategemea utoaji wa huduma ikiwamo utalii.

Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili Zisizorejesheka, Dk. Soud Nahoda, alitoa kauli hiyo jana alipofungua kongamano la kujadili mfumo wa chakula lilofanyika katika Chuo cha Utalii Maruhubi mjini Unguja.

Alisema kuwapo kwa mfumo mzuri wa chakula ni moja ya mabadiliko muhimu katika kufikia maendeleo ya mwanadamu, hivyo kongamano hilo litahamasishwa kasi ya mabadiliko ya dunia kwenye uzalishaji, ulaji na fikra kuhusu chakula na kusaidia kuandaa mwelekeo wa baadaye wa mfumo wa chakula na kuongeza nguvu za pamoja za kufika malengo yaliyokusudiwa.

Alisema Serikali ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ushirikiano mkubwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Maendeleo la Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN) wameandaa kongamano hilo la mfumo wa chakula ili kuungana na dunia katika uandaaji wa mpango wa mfumo wa chakula.

"Kongamano hili ninataka wananchi wote kushiriki katika kutoa maoni yenu ingawaje siyo rahisi kuwafikia watu wote, hivyo uwapo wetu hapa leo (jana) ni fursa kwenu ya kuwasilisha maoni ya wajasiriamali wengine waliobakia," alisema.

Dk. Nahoda alisema kongamano hilo limekuja baada ya kuonekana kuwa kuna tatizo ambalo linaendelea kukua siku hadi siku la kutokuwapo kwa mfumo sahihi wa utumiaji wa chakula katika jamii, hivyo kusababisha kuwapo kwa matatizo makubwa ya afya yanayotokana na lishe duni ikiwamo matatizo ya watoto kudumaa, uzito pungufu na ukosefu wa damu kwa mama wajawazito na wanaonyonyesha.

Alitoa angalizo kuwa mfumo wa chakula hauzungumzii tu uwapo wa mlo kamili, bali unagusa pia afya za wanyama na mazao yake, afya ya mimea na mazao yake, uchumi na uwezo wa kaya na sera mbalimbali.

Waziri huyo aliwataka washiriki wa kongamano hilo kutumia mbegu bora zinazostahamili ukame, maradhi na wadudu ili kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya hali ya hewa, kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira na kuweka mipango shirikishi ya matumizi sahihi ya ardhi na rasilimali za misitu.

Alisema kuwapo kwa ukaguzi wa mazao mashambani baada ya mavuno ili kumlinda mlaji, ukaguzi wa dawa zinazotumika katika kilimo na elimu ya kilimo ni muhimu kutolewa kuanzia shule za msingi.

Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa (UN) Zanzibar, Dorotry Temu Usiri, alisema mfumo wa chakula hugusa nyanja muhimu za maisha ya mwanadamu, mfano afya ya miili ya binadamu, mazingira, uchumi na tamaduni.

Alisema zinapofanya vizuri, mfumo wa chakula unaweza kuleta pamoja familia, jamii na taifa lakini kwa bahati mbaya mifumo mingi ya chakula ulimwenguni ni dhaifu, haijafanyiwa tathmini ya kutosha na ina hatari kuanguka na kutofikia malengo endelevu yaliyopangwa.

"Mifumo yetu ya chakula inaposhindwa upo uwezekano wa kuathiri sekta muhimu kama elimu, afya na uchumi na pia haki za binadamu, amani na usalama," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHARLES PATRICE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 144/0014** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary NSUMBA mwaka 1998, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kiuo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/336371/2021**

116346802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FAMILIA YA MAREHEMU HASSAN HAJI ALLY** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.750 DUQ** AINA YA **TOYOTA DAIHATS** RANGI YA BLUU.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBI/TR/RB/45/2021.**

116347602

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO. 53/2021**

**LENA WILSON.............................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**MUSA SADI ........................................................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
**KWA: MUSSA SADI,**

**Fahamu kwamba LENA WILSON amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.**

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 28/07/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. A Mapunda mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini.
Kumbuka: usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri shahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu wa Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 1/07/2021

A. Mapunda
MWENYEKITI
01/07/2021.

116347702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II (S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo........PONGWE**

**Usimamizi wa Mirathi..........27.........2021**

**Ombi la GULAMMOHAMED IBRAHIM ISMAIL Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu IBRAHIM ISMAIL PUNJA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20/7/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. arehe 25/6/2021.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

216348302

**NDG. AGGREY AMBANGILE NSEMWA**

Anatangaza kupotelewa na barua ya toleo la ofa **(letter of offer)** ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kiwanja **(new offer charges & land rent receipts) za kiwanja Na.2223 kitalu 'M', na Plot Na.2023 Block 'M'-Forest,Mbeya.**
Stakabadhi pamoja barua vilitolewa kwa mmiliki **Ndg. Aggrey Ambangile Nsemwa** wa S.L.P 2209, Mbeya na Halmashauri ya Jiji la Mbeya,chini ya sheria ya usajili ya Ardhi **(SURA 334).**
Kwa yeyote atakayeviona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi.

**TAARIFA YA POLISI:**
**MBE/MBE/RB/276129/2021**

Jacob Ngowi
**AFISA MTEULE**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.**

216348202

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDMUND TARIMO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0110/0028** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ILBORU** mwaka 1994,yeyote atakayekiokota atoe taarifs kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/335832/2021**

116346702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FARIS EXPRESS SERVICES COMPANY LIMITED** INATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 907 DSD** – TOWNACE NOAH. CHASSIS NAMBA **SR500090968.** ENGINE NAMBA **3S7916869.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/OST/RB/337020/2021.**

116346602

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.201/2021**

**Ombi la RACHEL FRANK MONGI Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu FRANK MICHAEL MONGI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shauri mnamo tarehe 09/07/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 06/07/2021

116346902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**WILAYA NYAMAGANA MWANZA**

**SHAURI LA MIRATHI NO 09 YA 2021**

**EDAH ISRAEL MATARI...........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**FESTO RUEBEN MATARI........................MAREHEMU**

**KWA YEYOTE YULE**
**POPOTE ALIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Mtajwa hapo juu amefungua maombi ya kuomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu FESTO RUEBEN MATARI mahakama hii imepanga kusikiliza shauri hilo mnamo tarehe 06/07/2021, saa 2:30 Asubuhi. Hivyo endapo kama kuna pingamizi lolote lile juu ya shauri hilo, liwasilishwe mahakamani tarehe tajwa hapo juu kabla mwombaji hajateuliwa na mahakama hii kuwa msimamizi wa mirathi.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 28/05/2021.

HAKIMU MKAZI
WILAYA YA NYAMAGANA
MWANZA

116347202

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 03/2019**

**RUTH JOHN MAKUNE.............................................MDAI**

**DHIDI YA**

**JOHANA MAKUNE SHILATU.........................MAREHEMU**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYO PEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO KWIMBA-MWANZA TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI YA MIRATHI SIKU YA IJUMAA TAREHE **06/08/2021** KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA. MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ILIPO

| S/N | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA, kiwanja na 30/31 kitalu "L" | MTAA WA UHURU, MWANZA. | SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYO FIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYO SALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE KUANZIA TAREHE YA MNADA, KUSHINDWA KUFANYIKA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

116347302

**MAWASILIANO.....0766-342969/0747-405464.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MILELE L. KIYUNGU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1856-0003** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BULUNGWA SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **NML/RB/312/2020.**

116348502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHINA CIVIL ENGINEERING CONSTRUCTION CORPORATION** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TRAILER yenye namba za usajili **T 316 AGN**, chasisi namba **DT 1111,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituochochotecha polisi

Polisi taarifa
**DAR/OST/RB/250403/2021**

116346502

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wanafunzi 150 watekwa nyara Nigeria

**Kaduna, NIGERIA**

WANAFUNZI 150 hawajulikani walipo baada ya watu waliokuwa na silaha kuvamia shule ya bweni katika jimbo la Kaduna nchini Nigeria.

Mzazi mmoja na ofisa tawala, wamesema juzi kuwa polisi pamoja na wanajeshi wanawasaka wanafunzi hao.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, shule hiyo ya sekondari ya Bethel Baptist ni ya 10 kushambuliwa Kaskazini Magharibi mwa Nigeria, tangu Desemba, mwaka jana.

Mamlaka zinasema kuwa washambuliaji hudai fidia baada ya kuwateka nyara wanafunzi.

Ripoti zinasema kuwa dazeni ya wazazi waliokuwa wakilia walikusanyika kwenye shule hiyo, wakitarajia kupata taarifa kuhusiana na waliko watoto wao.

Ripoti za polisi zinasema kuwa washambuliaji waliingia saa za usiku na kuwashinda nguvu walinzi waliokuwapo huku wakitoroka na wanafunzi kuelekea kwenye msitu ulio karibu.

Hata hivyo taarifa zilisema kuwa watu 26 akiwamo mwalimu mmoja wa kike wameokolewa.

Mwanzilishi wa shule hiyo Kasisi John Hayab, aliiambia Reuters kwamba takriban watu 25 walibahatika kuponyoka wakati wanafunzi waliobaki walishikwa mateka na washambuliaji.

***VOA***



Ndege ya abiria aina ya Antonov An-26 imepotea ikiwa na takribani watu 28, huku mamlaka za vyombo vya habari Urusi zikisema uwezekano ni mdogo kupatikana manusura. Tukio hilo lilitokea jana Mashariki mwa nchi wakati ndege hiyo ikifanya safari kutoka Petropavlovsk-Kamchatsky kuelekea Palana. **PICHA: BBC**

# Benki Kuu DRC yapata Gavana mpya mwanamke

**Kimshasa, DRC**

MALANGU Kabedi Mbuyi, ameteuliwa kuwa Gavana mpya wa Benki Kuu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (BCC).

Uteuzi huo unamaanisha kuwa taasisi hiyo nyeti ya kifedha DRC itaongozwa na mwanamke huyo, ambaye kabla ya kushika nafasi hiyo, alikuwa mwakilishi wa Shirika la Fedha (IMF), Burkina Faso.

Wachambuzi wa mambo wanasema, mabadiliko katika benki hiyo, yalikuwa muhimu kuendana na matakwa ya IMF kabla ya kuipa DRC mkopo wa Dola Bilioni 1.5.

Mbuyi anachukua nafasi ya Déogratias Mutombo, ambaye alionekana kuwa mshirika wa karibu wa Rais wa zamani Joseph Kabila aliyeshika nafasi hiyo tangu mwaka 2013.

Mabadiliko mengine yaliyofanyika ni kuondoka kwa Albert Yuma, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo.

Aidha, kwa mara ya kwanza, benki hiyo itakuwa na manaibu wawili wa magavana kwa mujibu wa mabadiliko yaliyofanyika mwaka 2018 na wawili hao ni washirika wa karibu wa Rais Felix Tshisekedi.

Wawili hao ni aliyekuwa Seneta Dieudonné Fikiri na mwanachama wa chama cha siasa UDPS William Pambu.

***RFI***

# Papa aanza mazoezi baada ya upasuaji

**Roma, ITALIA**

AFYA ya Papa Francis inaendelea kuimarika baada ya jana kupata kifungua kinywa, kusoma magazeti na kufanya mazoezi ya kutembea, ikiwa ni siku mbili baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuondoa sehemu ya utumbo mpana.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa Vatican. Msemaji wa Vatican alisema, Baba Mtakatifu Papa Francis alilala vyema usiku na leo (jana), asubuhi alikunywa chai, kusoma magazeti na kutembea.

Papa Francis, 84, alifanyiwa upasuaji wa kuondoa sehemu wa utumbo mkubwa 'colon' iliyochukua saa tatu kutokana na ugonjwa ujulikanao 'colon diverticulum stenosis', anatarajiwa kukaa hospitali kwa takribani wiki moja katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Gemelli.

Haijulikani ni kwa nini watu huugua ugonjwa huo, unaonekana kuhusishwa na umri, chakula, maisha mtu anayoishi na jeni.

Wenye umri mkubwa kwa asilimia 80 hukumbwa na tatizo hilo, na ni miongoni mwa sababu hatari zinazosababisha maradhi ya diverticular.

Watu wachache walio chini ya umri wa miaka 40 huugua maradhi haya. Hii ndio mara ya kwanza Papa Francis kulazwa hospitalini tangu uteuzi wake 2013.

Sababu nyingine zinazosababisha hatari ni pamoja na mtu kuongeza uzani, kuvuta sigara, kuwa na historia ya haja ngumu na matumizi ya muda mrefu ya dawa za kuondoa maumivu kama vile Aspirin.

Jumapili iliyopita Papa Francis alikuwa katika hali yake ya kawaida wakati akitoa baraka zake za kila wiki katika kanisa la Mtakatifu Peter.

Akiwa Buenos Aires, Argentina 1966, Papa Francis alipoteza upande mmoja wa pafu lake la kulia akiwa na umri wa miaka 21.

Pia aliugua tatizo la nyonga na sciatica ambayo hueneza maumivu mgongoni na miguuni.

Mwaka 2014, alilazimika kukatiza hafla nyingi kutokana na tatizo la tumbo, iliripotiwa.

**AP**

# Huawei kuchochea digitali Afrika

**Nairobi, KENYA**

JUMUIYA ya Mawasiliano ya Afrika (ATU) imetia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na kampuni ya Huawei, kuhakikisha nchi na mashirika ya Kiafrika yanajenga uwezo kwa ajili ya mabadiliko ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Katika makubaliano hayo, Huawei itatoa mafunzo ya kukuza ujuzi wa kidijitali kusaidia ubunifu wa ndani, kubadilishana habari kutatua na kuleta suluhisho kwa Afrika kuibuka kiuchumi na kuviunganisha vijiji.

Hatua hiyo inakuja huku ripoti ya mwaka 2019 ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Biashara na Maendeleo (UNCTAD) kuhusu uchumi wa kidijitali kuonyesha, Afrika na Amerika ya Kusini zinachangia chini ya asilimia tano ya vituo vya data duniani.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ni kwamba iwapo suala hilo litaachwa bila kushughulikiwa, kutakuwa na ongezeko la mgawanyiko kimapato usio sawa uliopo sasa kutokana na nchi zinazoendelea (LDCs), mtu mmoja kati ya watano anatumia intaneti, ikilinganishwa na watu wanne kati ya watano katika nchi zilizoendelea.

Akiongea wakati wa hafla ya utiaji saini iliyofanyika hivi karibuni jijini Nairobi, Kenya, katika makao makuu ya ATU, John Omo, Katibu Mkuu wa ATU, aliipongeza kampuni ya Huawei kwa mchango wake barani Afrika.

"Huawei imebadilisha muunganiko na imetoa mchango mkubwa barani Afrika kupitia uwekezaji wake katika miundombinu ya kidijitali ambayo ni rafiki kwa mazingira, kutoa ufundi wa ICT pamoja na teknolojia za hali ya juu kwa maeneo ya vijijini.

"Shirika hili ni mshirika wa maendeleo anayeaminika barani Afrika. Makubaliano tunayosaini yanalenga kuimarisha ushirikiano huu."

Aliongezea kwamba, Afrika ina nafasi kubwa ya kunufaika kutokana na teknolojia mpya.

Samuel Chen, Makamu wa Rais wa Huawei Kusini mwa Afrika, aliishukuru ATU kwa uongozi na uendelezaji wa ICT barani Afrika: "ATU inachukua jukumu muhimu kusaidia nchi wanachama katika sera na mikakati yao, kusaidiana uzoefu, kujenga uwezo na kuendesha ubunifu na tunafurahi kuweza kuwaunga mkono," alisema Chen.

"Tumeunganisha mamilioni ya Waafrika katika huduma salama, za kasi na za mtandaoni katika kipindi cha miongo miwili iliyopita na kupata uaminifu na msaada wa wateja wetu na wasimamizi. Tunatarajia kufanya hata zaidi."

Kulingana na makubaliano hayo, washirika wataanza kutoa mafunzo kwa ATU ambao watapata nafasi ya kushirikiana na wataalamu kujadili teknolojia na mwenendo wa mambo pamoja na kushirikiana kwenye utafiti kusaidia maendeleo ya kidijitali barani Afrika.



# PSG, MAN CITY ZAMGOMBEA MESSI

**PARIS, Ufaransa**

KLABU za Paris Saint-Germain na Manchester City zote zinafuatilia kwa makini hali ya usajili wa Lionel Messi baada ya mchezaji huyo sasa kuwa huru, kwa mujibu wa ukurasa wa kwanza kwa gazeti la Mundo Deportivo la jana, Jumanne.

Awali, iliripotiwa kwamba, Barcelona wamefikia makubaliano ya kumwongezea mkataba mpya nyota huyo wa Argentina baada ya kumaliza mkataba wake mwezi uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, mwaka jana alitangaza kutaka kuondoka pale Barcelona, lakini baadaye akaamua kubaki klabuni hapo.

Mkataba wa Messi pale Barcelona ulimalizika Juni 30, lakini inaonyesha anaweza asisaini tena kwa miamba hao wa LaLiga, ambao kwa sasa wapo kwenye matatizo ya kifedha.

Na sasa Mundo Deportivo limeripoti kuwa Messi bado hajafikia makubaliano na Barca na hivyo miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG na wale wa Ligi Kuu England, Man City zinamtolea macho.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or kwa sasa yupo na timu ya Taifa ya Argentina kwenye michuano ya Copa America.

## MAN UNITED YAJITOSA KWA CAMAVINGA

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imefungua mazungumzo rasmi na mawakala wa kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye miaka 18.

Baada ya kumsajili Jadon Sancho, Man United wanafanya kazi kusajili beki wa kati mpya na pia kiungo mpya msimu huu wa majira ya joto.

Camavinga anaangaliwa sana na bodi ya Man United kama mmoja wa malengo ya muda mrefu ya klabu hiyo.

Klabu ya Paris Saint-Germain pia imekuwa ikimfuatilia kwa muda mrefu kutaka kumsajili mchezaji huyo.

Lakini Man United wameanza mawasiliano ya moja kwa moja na Camavinga na Rennes wako tayari kujadili juu ya ada ya Euro milioni 30 kwani wanaweza kumpoteza mchezaji huyo bure katika kipindi cha majira ya joto.

Camavinga atamaliza mkataba wake Juni 2022 na mchezaji huyo hana haraka kuamua muskabali wake huku United na PSG wakiwa kipaumbele kumsajili mchezaji huyo.

## SPINAZZOLA AMPA PIGO MOURINHO



**LONDON, Italia**

NYOTA wa AS Roma na timu ya Taifa ya Italia, Leonardo Spinazzola atalazimika kukaa nje kwa miezi sita kutokana na majeraha ya kifundo cha mkono aliyoyapata wakati wa mechi ya robo fainali dhidi ya Ubelgiji.

Spinazzola alipata majeraha katika mechi hiyo ya robo fainali ambayo timu yake iliibuka na ushindi wa mabao 2-1, huku yeye kama beki akiwa katika ubora kwenye mechi hiyo kabla ya kutolewa nje kwa machela.

Mchezaji huyu amekuwa katika kipindi kizuri sana katika michuano hii ya Euro 2020 huku akiendelea kuonyesha ubora wake na kujihakikishia namba katika klabu yake iliyoangukia chini ya mikono ya Jose Mourinho.

Katika mechi za michuano ya Euro 2020, mchezaji huyo aliibuka kuwa mchezaji bora wa mechi mbili kati ya tano walizocheza.

Italia jana Jumanne ilikuwa inacheza na Hispania kwenye nusu fainali ya Euro 2020.



# LIVERPOOL

## YAJIPANGA KUMCHUKUA NIGUEZ

**LIVERPOOL, England**

RIPOTI mbalimbali nchini Hispania zinadai kwamba, Atletico Madrid imekubali kumuuza, Saul Niguez kwenda Liverpool msimu huu wa majira joto.

Jarida la La Razon, linaripoti kwamba, Liverpool wanamwona nyota huyo wa Atletico kama mbadala wa Gini Wijnaldum, ambaye alijiunga na PSG kwa uhamisho huru.

Hivi karibuni Times ilidai kwamba Saul Niguez anathamani karibu pauni milioni 60, lakini ripoti kutoka La Razon inadai kwamba Atletico wako tayari kumuachia kiungo huyo.


Liverpool sasa inaonekana kwamba, inaweza kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumnunua nyota huyo.

Klabu ilipo chini ya kocha Jurgen Klopp, inajipanga kuhakikisha inaimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Liverpool inahusishwa pia na usajili wa Yves Bissouma kutoka Brighton, Nicolo Barella wa Inter Milan, Otavio kutoka Porto na Ryan Gravenberch wa Ajax.

## BARCA KUWATOSA PJANIC, UMTITI

**BARCELONA, Hispania**



BARCELONA wameripotiwa kuwa wameruhusu nyota wao Miralem Pjanic na Samuel Umtiti, kuondoka klabuni hapo ili kupatikana fedha za usajili wa wachezaji wengine.

Kikubwa ni kwamba, fedha hizo pia ni kama sehemu ya kutaka kuhakikisha Lionel Messi anabaki klabuni hapo.

Wachezaji hao wote wawili wanaripotiwa kuwa hawapo kwenye mipango ya kocha Ronald Koeman.

Pjanic ameanza kwenye mechi sita pekee za LaLiga msimu uliopita tangu alipowasili kutoka Juventus huku Umtiti pi alipata fursa ya kuanza kwenye mechi sita tu hapo Barcelona.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Goal, klabu ya Barcelona inapanga kukaa kitako na wachezaji wote wawili na kukubaliana malipo ili waweze kuondoka kama wachezaji huru katika dirisha hili la uhamisho.

Barcelona kwa Messi ni kama nyumbani, amekuwapo klabuni hapo tangu akiwa na umri wa miaka 13 mwaka 2000.

Lakini mazungumzo ya kusaini mkataba mpya yamechukua muda mrefu na mpaka sasa inadaiwa ni suala la fedha tu ndiyo linawakwamisha Barca.

Taarifa zaidi zinabainisha kuwa Barca wanasaka kupunguza gharama za malipo ili waweze kumudu kumlipa Messi katika makubaliano ya mkataba mpya.

## RONALDO KUBAKI JUVENTUS




**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo nyota wa kikosi cha Juventus atasalia ndani ya kikosi hicho licha ya kuelezwa kwamba Real Madrid na Manchester United wanahitaji saini yake.

Msimu uliopita nyota huyo ilibaki kidogo aondoke kwa kuwa alikuwa anatajwa kuelekea Manchester United ambao walikuwa wanatajwa kuiwinda saini ya nyota huyo.

Wakala wa mchezaji huyo, Jorge Mendes, inaelezwa kuwa ameomba nyota huyo aongezewe mkataba ndani ya kikosi hicho cha Juventus.

Mkataba wake ndani ya Juventus umebakiza mwaka mmoja kwa kuwa alisaini dili la miaka mitatu akitokea Real Madrid na Mei mwaka huu ilikuwa inaelezwa kwamba alikuwa anafanya mazungumzo na Kocha Mkuu wa Manchester United, Ole Gunnar Solksjaer ili amrudishe ndani ya Old Trafford.

Msimu uliopita raia huyo wa Ureno alifunga jumla ya mabao 36 katika mechi 44 ambazo alicheza ndani ya Juventus.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MAGUIRE AIPA USHINDI ENGLAND KWA DENMARK

Kiakili tupo sawa kabisa, hivyo ninaimani tunakwenda kuwa bora zaidi kuliko...

**LONDON, England**

ENGLAND ina kikosi bora zaidi kwa sasa kuliko kile kilichopoteza dhidi ya Croatia kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 na kina imani kubwa kuifunga Denmark kwenye nusu fainali ya Euro 2020 leo, kwa mujibu wa Harry Maguire.

Simba watatu hao walipata ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Ukraine Jumamosi iliyopita katika robo fainali ya Euro 2020 jijini Roma, Italia – ukiwa ni ushindi wao mkubwa zaidi kwenye hatua ya mtoano katika mashindano makubwa na leo Jumatano watacheza dhidi ya Denmark pale kwenye Uwanja wa Wembley.

England katika nusu fainali yao ya hivi karibuni kwenye mashindano hayo, ilipoteza kwa Ujerumani kwa changamoto ya mikwaju ya penalti mwaka 1996, huku ikifungwa na Croatia kwenye Kombe la Dunia miaka mitatu iliyopita na ikamaliza nafasi ya nne.

Tangu ilipotwaa Kombe la Dunia mwaka 1966, England haijawahi kutinga fainali ya mashindano makubwa, lakini Maguire amesisitiza watatumia maumivu hayo ili kushinda kwenye nusu fainali ya leo.

"Hamasa ni kubwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari jana.

"Ni nusu fainali ya mashindano ya Ulaya. Kupoteza kwenye nusu fainali ya Kombe la Dunia kulituumiza sana.

"Tunatakiwa kuhakikisha kwamba kesho (leo), Jumatano tunamaliza hasira za kufungwa na Croatia.

"Nafikiri tuko bora zaidi kuliko tulivyokuwa mwanzo. Uzoefu ni kwamba tumejifunza mengi na tunajua kwamba tunahitaji kushinda.

"Tumekuwa na mechi nyingi kubwa kwa wakati huu na tunatakiwa kuimarika zaidi na tumekuwa pamoja kwa muda mrefu, kuanzia kwenye mechi za kirafiki hadi za kufuzu.

"Katika kila mchezo tumecheza kwa kuimarika zaidi na ninaamini tutakuwa bora sana.

"Kiakili tupo sawa kabisa, hivyo ninaimani kwamba tunakwenda kuwa bora dhidi ya Denmark kuliko tulivyokuwa dhidi ya Croatia.

"Tumekuwa kwenye nusu fainali mwaka 2018 katika Kombe la Dunia na naamini sasa tutakuwa bora zaidi."

## KWA UFUPI

**RAMOS RASMI PSG**

MLINZI wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 35, jana Jumanne alifanyiwa vipimo vya afya jijini Paris kabla ya kujiunga na Paris St-Germain kama mchezaji huru kutokana na kuondoka Real Madrid. **(ESPN)**

**COMAN KUBAKI BAYERN**

MTENDAJI wa Bayern Munich, Oliver Kahn, ana uhakika wa kumbakiza klabuni hapo winga Mfaransa, Kingsley Coman licha ya Liverpool kuonyesha nia ya kumtaka nyota huyo mwenye umri wa miaka 25. **(Mirror)**

**VARANE HUYO UNITED**

KLABU ya Manchester United inajiandaa kutoa dau la pauni milioni 50 kwa ajili ya mlinzi wa Real Madrid, Mfaransa Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28. **(Marca via Mail)**

**BALOTELLI ATAKIWA UTURUKI**

MSHAMBULIA wa zamani wa Manchester City, Mario Balotelli mwenye umri wa miaka 30, anajiandaa kujiunga na klabu ya Adana Demirspor ya Uturuki, akiwa na imani ya kurejea kwenye timu ya taifa kwa ajili ya fainali za mwakani za Kombe la Dunia. **(Goal)**

**PSG YAMPA MESSI OFA**

KLABU ya Paris St-Germain imempa ofa Lionel Messi baada ya mkataba wake na Barcelona kukoma wiki iliyopita. Gwiji huyo wa Nou Camp mwenye umri wa miaka 33, ameisaidia nchi yake kufuzu nusu fainali ya Copa America licha ya sintofahamu ya mustakabali wake. **(Mail)**

**GRIEZMANN HUYO MAN CITY**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Mfaransa Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30, anaonekana kuwa chaguo linalowezekana kwa Manchester City msimu huu, iwapo City watashindwa kumnasa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. **(Mundo Deportivo)**

**POGBA KUREJEA JUVE**

JUVENTUS wanataka kumrejesha kiungo wake wa zamani anayeichezea Manchester United, Paul Pogba, 28, msimu huu. Wakali hao wa Italia wanataka kumrejesha Turin mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ikiwa ni miaka mitano tangu aondoke kwa uhamisho ulioweka rekodi ya dunia. **(90Min)**

**LIVER POA KWA MBAPPE**

LIVERPOOL inaongoza harakati za majaribio ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa na PSG, Kylian Mbappe. Tetesi zinaendelea kuhusu mustakabali wa kinda hilo lenye miaka 22, ambaye amebakiza mwaka mmoja tu wa mkataba wake pale Parc des Princes. **(ESPN)**

**VIEIRA AMTAKA CHRISTIE**

KOCHA mpya wa Crystal Palace, Patrick Vieira ana matumaini kwamba kiungo wa Scotland na Celtic, Ryan Christie atakuwa na usajili wake wa kwanza pale Selhurst Park. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 anawaniwa pia na klabu ya zamani ya Vieira, Nice. **(Daily Record)**

**ARTETA KUMBAKIZA ROWE**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ana uhakika wa kumbakiza Emile Smith Rowe pale Emirates licha ya ushawishi mkubwa kutoka Aston Villa. Villa inajiandaa kuongeza dau kwa ajili ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 20, baada ya lile la mwanzo la pauni milioni 30 kukataliwa. **(Mirror)**

## HABARI MICHEZO

### DIAMOND, WIZ KHALIFA JIKONI KUACHIA ALBAMU

**Haika Christopher na Ayubu Mpanja, SJMC**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Naseeb Abdul, maarufu Diamond Platnumz, yuko Marekani kwa ajili ya kutengeneza albamu yake mpya, akimshirikisha msanii mkali Wiz Khalifa.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram jana, Diamond aliweka picha yake akiwa na Wiz khalifa, ikisindikizwa na ujumbe uliosomeka "Wasafi × Taylor Gang".

Miaka sita iliyopita, Wiz Khalifa, msanii anayekimbiza kwenye mitandao ya kijamii kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi duniani, aliachia 'ngoma' aliyoiita 'See You Again' ambayo ilitazamwa na takribani mara bilioni tano kwenye mtandao wa YouTube.

Mbali na picha ya Wiz Khalifa, siku nne zilizopita, Diamond aliweka kipande kifupi cha video kwenye mtandao wa Instagram akiwa studio na msanii Busta Rhymes na baadaye alionekana kwenye picha na mtayarishaji wa muziki, Swizz Beats, mume wa msanii mkali Alicia Keys.

Julai 3, mwaka huu, kupitia ukurasa wake wa Instagram, Diamond alitangaza kuwa Rapa Swae Lee atahusika pia kwenye albamu yake hiyo anayoisuka.

### KATWILA APANIA SITA KWA YANGA, KMC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amesema anatambua ushindani ni mkubwa hususan mechi hizi za mwishoni mwa msimu, jambo ambalo amewataka wachezaji wake kujituma na kucheza bila kukata tamaa katika michezo yao miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobaki.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema hakuna mechi rahisi kwa upande wake, hivyo wanajipanga kuhakikisha wanapata pointi sita dhidi ya Yanga na KMC FC.

"Matumaini yangu ni kwamba hatushuki daraja, hizi mechi mbili tunahitaji kupigana na wachezaji wasikate tamaa ili kuhakikisha tunapigana hadi hatua ya mwisho kutafuta matokeo chanya katika michezo yetu hiyo," alisema Katwila.

Ihefu ambayo Julai 14 itacheza dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya Julai Julai 18, mwaka huu kumaliza na KMC FC kwenye Dimba la Uhuru Dar es Salaam, ipo nafasi ya nne kutoka mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 35.

# MAFUNZO YAIFUATA KMKM KUIWAKILISHA ZANZIBAR CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

RASMI sasa timu ya Mafunzo ndiyo itakayoiwakilisha Zanzibar baada ya kutwaa Kombe la Michuano la Shirikisho la Soka visiwani hapa (ZFF) maarufu FA Cup, kwa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya mabingwa watetezi, KVZ.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Amaan juzi, timu hizo zilifikia changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya kutoshana nguvu kwa kufungana bao 1-1 ndani ya dakika 90.

KVZ ndiyo ilikuwa ya kwanza kupata bao kupitia kwa Nassor Salehe dakika ya 13 kabla ya Abdulkadir Naimu kuisawazishia Mafunzo dakika ya 34 kupitia mpira wa adhabu ndogo.

Baada ya kukamilika dakika 90, ilibidi kufanyika majadiliano kwa dakika kadhaa kati ya timu hizo, ZFF waamuzi wa mchezo huo kabla ya kukubaliana kwenda moja kwa moja kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti.

Kwa matokeo hayo Mafunzo sasa itaiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika huku timu ya KMKM iliyotwaa ubingwa wa Ligi Kuu, ikibeba jukumu hilo kwa upande wa michuano Ligi ya Mabingwa Afrika.

Michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), inatarajiwa kuanza rasmi mapema Septemba mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Mafunzo, Abdalla Bakari "Edo", aliwapongeza wachezaji wake na benchi la ufundi katika kutimiza ndoto yao ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Alisema wachezaji wake walifanya kazi nzuri na mashabiki pia walisaidia katika kuongeza hamasa kwao kuhakikisha wanachukua kombe hilo.

"Tunashukuru lengo letu limetimia, hii ni furaha kwetu, maana mara ya mwisho kushiriki mashindano haya ilikuwa mwaka 2016, hivyo hii ni zawadi muhimu na tunakwenda kujipanga mapema," alisema.

Edo alisema lazima wahakikishe wanafanya maandalizi ambayo yataleta mafanikio kwa upande wa michuano ya kimataifa na hata Ligi Kuu Zanzibar kuelekea msimu mpya.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, baada ya kuwasili katika ofisi za kampuni hiyo jijini Dar es Salaam kwa ziara maalum. Wapili kushoto ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa nchini, Dk. Emmanuel Ishengoma na kulia ni Mkuu wa Uhusiano wa MultiChoice Tanzania, Johnson Mshana. **MPIGAPICHA WETU**

# Bashungwa aipongeza DStv kukuza filamu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa amewahakikishia wadau wa sekta zilizo chini ya wizara yake ushirikiano wa karibu ili kuhakikisha ukuaji thabiti wa sekta hizo na kuongeza mchango wake katika maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Bashungwa ameyasema hayo wakati wa ziara yake katika Ofisi za MultiChoice Tanzania - DStv, ziara ambayo ilikuwa na lengo la kufahamu zaidi utendaji wa kampuni hiyo katika kukuza sekta ya sanaa hususan tasnia ya filamu hapa nchini.

Katika ziara hiyo Waziri Bashungwa aliambatana na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa, Dk. Emmanuel Ishengoma na Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo.

Akizungumza na uongozi wa MultiChoice Tanzania pamoja na baadhi ya wazalishaji wa filamu nchini, Bashungwa ameipongeza Kampuni ya MultiChoice kupitia chaneli zake za DStv kwa kuwa kinara katika kukuza tasnia ya filamu nchini.

Waziri huyo alisema kitendo cha DStv kuwa na chaneli maalum kwa ajili ya maudhui ya Tanzania – Maisha Magic Bongo, ni ishara tosha kuwa kampuni hiyo inatilia maanani maudhui ya ndani na kwamba serikali iko tayari muda wote kutoa ushirikiano unaohitajika kwa wadau ili kuhakikisha kuwa tasnia ya sanaa nchini inakuwa chanzo muhimu cha ajira na kukuza uchumi kwa ujumla.

Aidha, Bashungwa alikemea vikali vitendo vya uharamia wa maudhui (content piracy) na kusema kuwa atashauriana na mamlaka na idara nyingine zinazohusika ili kuhakikisha kuwa suala hilo linashughulikiwa.


Bashungwa pia amekiagiza Chama cha Haki Miliki Tanzania (COSOTA), kuhakikisha kuwa wanaongeza nguvu katika mapambano dhidi ya uharamia wa maudhui na wote wanaobainika kufanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua kali.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, alitoa shukrani za kampuni hiyo kwa wizara na waziri binafsi kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa kampuni hiyo na kwamba kitendo chake cha kufanya ziara hiyo ni ishara tosha kuwa serikali inaheshimu sana mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya sekta ya habari nchini.

Woiso amemhakikishia waziri huyo na Watanzania kwa ujumla kuwa, DStv itaendelea kuimarisha maudhui ya Tanzania katika chaneli zake huku ikihakikisha kuwa inatoa mchango mkubwa katika uboreshaji na uimarishaji wa maudhui ya ndani ili yawe katika viwango vya kimataifa na kuweza kushindana katika soko la maudhui.

# Michezo

Jumatano Julai 7, 2021
Nipashe



MAGUIRE AIPA USHINDI ENGLAND KWA DENMARK HABARI UK 22

NAMNA HII..



Winga wa Simba, Bernard Morrison, akimiliki mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo ambayo leo itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuvaana na KMC FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: SIMBA**

# KMC yaitishia Simba kwa mbinu za Yanga

●●● Ni wakati zikivaana leo, yatamba kutokubali kuwa daraja kwa kutafuta bao la mapema kisha...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

USHINDI ndio neno pekee ambalo limekuwa likitajwa na timu mbili, Simba na KMC FC kuelekea mchezo wao wa leo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Simba inashuka dimbani ikitoka kujeruhiwa Jumamosi na Yanga na kushindwa kufikia malengo yao ya kutangaza ubingwa mapema kwa mara ya nne mfululizo.

Wakati Simba wakihitaji kumaliza hasira zao kwa kupata pointi tatu ili kufikisha alama 76 na kijiweka katika mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ambayo bingwa huiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, KMC FC wao wanashuka dimbani wakifikiria zaidi kupata ushindi ili kuisaka nafasi ya nne na kujiweka katika mazingira mazuri ya kuwa miongoni mwa timu nne zitakazoshiriki michuano ya kimataifa.

Wakizungunza na gazeti hili, makocha wa timu hizo, kwa upande wa Simba, Kocha Msaidizi, Selemani Matola, alisema mechi dhidi ya KMC si rahisi lakini wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi tatu ambazo zitawawezesha kufikia malengo yao ya kutangazwa bingwa.

"Tumefanyia kazi upungufu wetu uliojitokeza katika mechi iliyopita, si mechi rahisi kwa sababu KMC ina wachezaji wazuri, hata sisi tumejipanga kwenda kutafuta pointi tatu katika mechi hiyo," alisema Matola.

Alisema hakuna mchezaji anayekosa katika mchezo huo kwa sababu wote walioku-wapo katika kikosi hicho wako fiti na sasa wanasubiri kwenda uwanjani kutafuta pointi.

Kuhusu kutoonekana kwa kocha wa makipa wa Simba, Milton Nienov, Matola alisema hatakuwa sehemu ya benchi la ufundi baada ya kwenda kwao Brazil kwa ajili ya kufanya mtihani wa kumaliza kozi aliyokuwa akisoma. Kocha wa KMC FC, Habibu Kondo, alisema wamejiandaa vizuri na haijalishi Simba ametoka kupoteza, wanaangalia zaidi kupata matokeo mazuri ili kufikia malengo yao ya kumalizana na ligi wakiwa katika nafasi nne za juu.

Alisema walipoteza mechi ya kwanza mbele ya Simba na sasa hawatakuwa tayari kuona wanafungwa kwa mara ya pili, hivyo wanakwenda kutafuta matokeo chanya.

"Tunaenda uwanjani kufanyia kazi 'Plan' yetu kuhakikisha tunapata matokeo ili kumaliza ligi katika nafasi ya nne, lazima tushinde dhidi ya Simba ili kufikia malengo hayo ya kuwa miongoni mwa timu zitakazoshiriki michuano ya kimataifa," alisema Habibu Kondo.

Awali, Kondo aliliambia Nipashe: "Nimeiangalia Simba, tutatumia udhaifu ule ule ambao inao na iliotokea dhidi ya Yanga. Tutawapiga presha tangu mwanzo wa mchezo na nina hakika kuwa tutawachanganya na kupata bao kama ilivyokuwa kwa Yanga."

Iwapo Simba inayoongoza ligi kwa pointi 73, ikishinda itafikisha pointi 76 ambazo Yanga ndiyo timu pekee itakayoweza kuzifikisha kama ikishinda mechi mbili ilizobakiza. Wakati huo Simba itakuwa imebakisha mechi tatu, ikihitaji pointi moja tu kutwaa ubingwa.

KMC ambayo ilipoteza mechi ya mzunguko wa kwanza dhidi ya Simba kwa bao 1-0 lililofungwa na Meddie Kagere kwa mkwaju wa penalti, inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 42, ikishinda itafikisha pointi 45 na kuipiku Namungo FC yenye pointi 43, ikiwa kwenye nafasi ya tano.

## NABI AIWAISHA YANGA KAMBINI

**Na Saada Akida**

BAADA ya mapumziko ya siku mbili, kikosi cha Yanga kinaingia kambini leo, Jumatano tayari kwa kujiwinda na michezo miwili ya kuhitimisha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 dhidi ya Ihefu FC na Dodoma Jiji FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema wamerejea kambini kujiandaa na michezo hiyo miwili kutafuta pointi sita ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kupambania ubingwa.

Alisema anaridhishwa na mabadiliko ya timu yake kwa wachezaji kupambana na sasa anafanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita ili kuweza kufikia malengo yao katika mechi hizo mbili.

"Bado tuna nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, nina jivunia wachezaji wangu ambao hujitolea kutafuta matokeo, mechi zilizobaki si rahisi, tunahitaji kupambana na kushinda ili tumalize ligi tukivuna pointi sita," alisema Nabi.

Yanga ambayo mchezo uliopita iliwafunga watani zao wa jadi kwa bao 1-0, ipo katika nafasi ya pili ikiwa na pointi 70, tatu nyuma ya vinara Simba waliobakiza mechi nne. Mchezo ujao Yanga itaikaribisha Ihefu FC Julai 14, mwaka huu katika Uwanja wa Mkapa.

Mbali na mechi hiyo ya Ligi Kuu, pia Yanga inakabiliwa na kibarua kigumu cha kuhakikisha msimu huu inamaliza na taji, kutokana na kutinga fainali ya Kombe la FA ambapo itavaana na Simba Julai 25, mwaka huu katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Hata hivyo, itacheza mechi hiyo ikiwa na ari ya ushindi kutokana na matokeo ya bao 1-0 iliyoyapata kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya watani zao hao, Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002